# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la 4



Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Nne



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 558

Jina la Chapisho: Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-326-7

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Nne katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

©Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018

Toleo la Pili 2021

ISBN 978–9987–09–326–7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 170 / +255 735 041 168

Barua pepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 2 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**........................................................................ v

**Shukurani**........................................................................vi

**Sura ya Kwanza**

Mazingira yetu...................................................................1

**Sura ya Pili**

Matukio ya kihistoria........................................................14

**Sura ya Tatu**

Hali ya hewa.....................................................................27

**Sura ya Nne**

Utamaduni wetu................................................................38

**Sura ya Tano**

Uhusiano mwema katika jamii.......................................... 47

**Sura ya Sita**

Mashujaa wetu..................................................................68

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 3 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Saba**
Kutumia ramani katika mazingira......................................84

**Sura ya Nane**
Mfumo wa jua.............................................................96

**Sura ya Tisa**
Rasilimali zetu..........................................................108

**Sura ya Kumi**
Uzalishaji mali..........................................................118

**Sura ya Kumi na Moja**
Fursa katika maeneo mbalimbali....................................129

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 4 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu cha Maarifa ya Jamii Darasa la Nne ni kitabu cha pili cha mwanafunzi katika mfululizo wa vitabu vya somo hili. Uandishi wa kitabu hiki umezingatia mahitaji ya mwanafunzi katika kukuza na kuendeleza umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Kitabu kimeandikwa ili kutambua matukio katika mazingira na misingi ya uzalendo, namna ya kutumia ramani na elimu ya anga, na kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali. Mada kumi na moja zinazounda kitabu hiki zimeandaliwa ili kumsaidia mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa katika somo la Maarifa ya Jamii Darasa la Nne.

Ili kukidhi mahitaji hayo, kila mada imesheheni matini za kusoma. Matini hizo zimeandikwa kwa mtindo wa ushairi, majigambo, nyimbo, hadithi, majibizano na vifungu vya maneno vyenye kufafanuliwa kwa picha na michoro.

Maswali yaliyomo kwenye kitabu hiki katika muundo wa mazoezi na kazi za kufanya yatamwezesha mwanafunzi kufikiri na kujenga umahiri uliokusudiwa. Aidha, kazi za kufanya zitamwezesha kupata uelewa wa kina na kuutumia umahiri uliojengwa katika maisha yake ya kila siku.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 5 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la “Global Partnership for Education (GPE)” kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao “Literacy and Numeracy Education Support (LANES)” kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi Ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 6 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Mazingira yetu

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza vitu vinavyounda mazingira ya shule na pia ulifanya usafi wa darasa. Pia, ulijifunza namna ya kupanda maua, nyasi na miti katika mazingira ya shule. Katika sura hii, utajifunza mazingira ya kijijini na mjini. Vilevile, utajifunza vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira ya kijiji, mtaa na mji. Pia, utajifunza shughuli za utunzaji wa mazingira ya mtaa, kijiji na mji.

### Maana ya mazingira

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyotuzunguka. Mazingira huundwa na vitu mbalimbali. Vitu hivyo vinaweza kuwa vya asili kama misitu, milima, maziwa, mabonde, mito, wanyama na bahari. Pia, vipo vitu vilivyotengenezwa na binadamu kama vile majengo, barabara na viwanda. Vyote hivi huunda mazingira ambayo hupatikana maeneo ya kijijini au mjini. Sisi binadamu pia ni sehemu ya mazingira.

### Mazingira ya kijijini na mjini

Bila shaka umewahi kuona au kuishi kwenye nyumba ya bati au nyasi. Pia, umewahi kuketi chini ya mti wenye kivuli. Tena umewahi kuona sehemu zenye mashamba ya mazao na mabomba ya maji. Vilevile, utakuwa umewahi kuona mito, misitu, wanyama, milima na mabonde. Hivi vyote ni sehemu ya mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 1 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 1:** *Mazingira ya kijijini*




**Kielelezo namba 2:** *Mazingira ya mjini*

## Zoezi la 1

1. Ni vitu gani vinavyounda mazingira ya kijijini na mjini kama vinavyoonekana katika picha?
2. Ni vitu gani vinavyopatikana katika mazingira ya mtaa au kijiji unachoishi lakini havionekani katika picha?
3. Kuna tofauti gani kati ya vitu vilivyopo kwenye mazingira ya kijijini na mjini?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 2 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari hii, kisha jibu maswali.**

Kila mmoja wetu anaishi katika kijiji au mtaa fulani. Kijiji ni eneo lililoko nje ya mji. Kila kijiji huundwa na vitongoji kadhaa. Kijiji huwa na serikali yake inayoongoza watu waliomo katika kijiji hicho. Mazingira ya kijiji hutofautiana kulingana na maendeleo yaliyofikiwa. Katika mazingira ya kijijini kunaweza kuwa na mapori. Baadhi ya mapori huwa na wanyama kama tembo, simba, chui na fisi. Pia, katika maeneo ya vijijini kuna mashamba. Vilevile, wapo wanyama wa kufugwa kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Tofauti na kijiji, mtaa ni sehemu ndogo ya mji yenye makazi ya watu. Mitaa kadhaa huunda kata. Mtaa pia huwa na serikali yake ya kuongoza watu waliomo. Mazingira ya mjini pia huundwa na vitu mbalimbali. Vitu vinavyounda mazingira ya mjini ni majengo ya kisasa yaliyoezekwa kwa vigae au bati. Baadhi ya majengo hayo ni ya ghorofa. Pia, katika mazingira ya mjini kuna viwanda vingi vya aina mbalimbali.

Katika mitaa ya mjini yapo maduka makubwa ya bidhaa mbalimbali. Vilevile, kuna vyombo vya usafiri kama vile magari na ndege. Pia, hospitali, shule, vituo vya polisi na viwanja vya ndege hupatikana zaidi mijini kuliko vijijini. Mazingira ya mjini na kijijini hutofautiana kwa mandhari yake.

**Zoezi la 2**

1. Kitu gani kilichokuvutia katika habari uliyoisoma?
2. Taja huduma tatu za jamii zinazopatikana mjini kutoka kwenye habari uliyosoma.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 3 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Ni vitu gani ambavyo havijatajwa katika habari vinavyopatikana katika mazingira ya mtaa au kijiji unachoishi?
4. Ni huduma gani za jamii zinazopatikana kijijini au mtaani kwako?

**Kazi ya kufanya**

Shirikiana na wanafunzi wenzako na mwalimu wa somo kufanya mambo yafuatayo:

(a) Kama shule yako ipo kijijini fanya ziara ya kutembelea mazingira ya mjini.

(b) Kama shule yako ipo mjini fanya ziara ya kutembelea mazingira ya kijijini.

(c) Chunguza vitu vinavyounda mazingira husika, kisha andika vitu hivyo na kuwasilisha kwa wenzako.

## Uharibifu wa mazingira

Yapo maeneo yenye mazingira mazuri ambayo hayajaharibiwa. Pia, yapo maeneo mengine ambayo mazingira yake yameharibiwa.

Binadamu hufanya shughuli mbalimbali ambazo baadhi yake husababisha uharibifu wa mazingira. Shughuli hizo ni pamoja na uchomaji wa mkaa. Shughuli nyingine ni ujenzi holela na utupaji taka ovyo. Pia, shughuli za viwanda kama vile utiririshaji maji yenye kemikali katika mito, maziwa na bahari. Vilevile, moshi hasa wa viwandani husababisha uchafuzi wa hewa. Mazingira yaliyoharibiwa hayafai kwa shughuli za kilimo wala makazi. Pia, husababisha maradhi kwa binadamu, mifugo na viumbe wengine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mazingira yaliyoharibiwa huweza kurekebishwa kwa kupanda nyasi na miti. Nyasi na miti hupandwa sehemu zenye mmomonyoko wa udongo na zilizokosa miti. Pia, kulima kilimo cha matuta ya kukinga maji kwenye miteremko. Vilevile, kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti. Hali kadhalika, mazingira machafu husafishwa kwa kufyeka vichaka, kuondoa taka sehemu za makazi na kuzihifadhi kwenye vyombo sahihi na sehemu zinazotakiwa.

*Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



b.






Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 5 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

c.



**Kielelezo namba 3:** *Shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira*

## Zoezi la 3

1. Ni vitendo gani vimesababisha uharibifu wa mazingira katika picha?
2. Ni madhara gani yatatokea kama uharibifu wa mazingira ukiendelea?
3. Taja vitendo vitatu vya uharibifu wa mazingira vinavyofanyika mtaani au kijijini kwako.
4. Unafikiri ni kwa nini vitendo hivi vinafanyika?
5. Je, ukikuta mtu anaharibu mazingira ya sehemu unayoishi, utachukua hatua gani?

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wanafunzi wenzako, kutembelea kijiji au mtaa karibu na shule yenu. Kisha chunguza na kubainisha:

(a) Shughuli zinazofanyika katika eneo hilo.

(b) Shughuli yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira. Kisha andika taarifa ya shughuli hiyo kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 6 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali.**

Jamina alikuwa akiishi na wazazi wake katika Kijiji cha Kilimani. Jamina alipenda kushiriki katika shughuli za utunzaji wa mazingira pale kijijini kwao. Baadaye, jamii ya wafugaji ilihamia na mifugo yao pale kijijini. Hali hii ilisababisha idadi ya watu na mifugo kuongezeka. Watu wakaanza kulima na kujenga kando kando ya mto. Pia, wakaanza kulima kwenye miteremko bila kutumia matuta ya kukinga maji. Mifugo nayo ilikuwa mingi kuliko eneo la malisho.

Kwa kuwa ujenzi wa nyumba ulihitaji mchanga, watu wengi walichimba mchanga pembezoni mwa mto. Hali kadhalika, ukataji miti uliongezeka mno. Miti ilitumika kwa malengo mbalimbali kama vile ujenzi, kupata kuni na kuchoma mkaa. Hali hii ilisababisha msitu uliokuwepo kutoweka kwa kasi. Kutoweka kwa msitu kulisababisha mazingira ya Kijiji cha Kilimani kuharibika.

Siku moja, Jamina alikwenda kumtembelea shangazi yake huko mjini. Jamina alidhani mjini hakuna vitendo vinavyoharibu mazingira. Alipofika mjini alishangaa sana alichokiona na kusema kimoyomoyo; "*Ha! Kumbe hata mjini kuna uharibifu wa mazingira!*" Jamina alishangaa kuona takataka zikiwa zimetupwa ovyo katika maeneo mbalimbali. Mitaro ilitiririsha maji machafu katika makazi ya watu na barabarani. Pia, maeneo mengi yalikuwa na usumbufu wa kelele zilizotokana na shughuli za gereji na karakana. Vilevile, kelele zilitokana na wafanyabiashara ndogondogo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maisha ya kijijini na mjini yalimnyima raha Jamina. Hii ilimpa msukumo wa kutaka kujifunza zaidi kuhusu mazingira. Jamina aliamini kuwa elimu hiyo ingemsaidia kuelimisha watu juu ya utunzaji wa mazingira. Jamina alipomaliza elimu ya sekondari alijiunga na Chuo cha Mazingira. Katika chuo hicho, Jamina alisomea kozi za usimamizi wa mazingira.

## Zoezi la 4

1. Kisa ulichosoma kinataja vitendo gani vinavyoharibu mazingira? Jibu kwa kujaza nafasi zifuatazo.

| Na | Kijijini | Mjini |
|---|---|---|
| (a) | | |
| (b) | | |
| (c) | | |
| (d) | | |
| (e) | | |

2. Kitu gani ulichojifunza kutoka kwenye habari hii?
3. Unadhani uamuzi wa Jamina ulikuwa sahihi? Kwa nini?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matokeo ya uharibifu wa mazingira




**Kielelezo namba 4:** *Athari za kuharibu mazingira*

**Kazi ya kufanya**

Chunguza mazingira ya kijiji au mtaa unaoishi na andika madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira. Kisha wasimulie wenzako darasani.

## Utunzaji wa mazingira

Utunzaji wa mazingira ni hali ya kutunza, kulinda na kuhifadhi jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu katika maisha yake. Vitu hivyo ni kama vile mito, mabonde, wanyama, milima na bahari.

Shughuli za utunzaji wa mazingira katika nchi hufanyika katika ngazi mbalimbali. Serikali yetu ilianzisha taasisi na ofisi za kusimamia utunzaji wa mazingira. Zipo ofisi za mazingira ngazi



FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 9 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya kijiji, mtaa na kata. Pia, zipo katika ngazi ya wilaya, mkoa, kanda na taifa. Ofisi hizi husimamiwa na maofisa mazingira katika ngazi mbalimbali. Maofisa hao hushirikiana na viongozi wa serikali katika utunzaji wa mazingira.

Aidha, kwa kila ngazi husika kuna kamati mbalimbali za utunzaji wa mazingira. Kamati hizo ni pamoja na zile za afya na mazingira. Kamati hizi hufanya kazi za kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za utunzaji wa mazingira. Shughuli hizi ni pamoja na kupanda miti na kuitunza. Ni jukumu la kila serikali ya ngazi husika kuwa na sheria ndogondogo pamoja na faini kwa kila atakayebainika amechafua mazingira. Mfano, katika baadhi ya maeneo faini ni shilingi elfu hamsini. Tunapaswa kutunza mazingira yetu ili kulinda maisha yetu na viumbe wengine.

*Angalia picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*




**Kielelezo namba 5:** *Elimu ya kutunza mazingira*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Unajifunza nini kutokana na picha unayoiona?
2. Taja shughuli tatu za utunzaji wa mazingira ulizozisoma kwenye picha.
3. Taja shughuli mbili nyingine za utunzaji wa mazingira ambazo hazijaandikwa kwenye picha.

### Kazi ya kufanya

(a) Panda maua nyumbani kwa kuzingatia hatua zifuatazo:
   (i) Tengeneza tuta la kupanda maua au jaza udongo kwenye chombo ambacho unaweza kupanda maua,
   (ii) tafuta miche ya maua,
   (iii) panda miche hiyo,
   (iv) endelea kumwagilia miche hiyo.

(b) Andika sentensi tano kueleza namna ambavyo wewe na wenzako mnavyotunza mazingira ya shule yenu.

(c) Tembelea ofisi ya serikali ya kijiji au mtaa iliyo karibu na eneo lako. Kusanya taarifa kuhusu shughuli za utunzaji wa mazingira zinazofanyika hapo mtaani au kijijini. Wasilisha kuhusu taarifa hiyo darasani kwako.

## Faida za utunzaji wa mazingira

Soma shairi lifuatalo ili kubaini faida za utunzaji wa mazingira ya kijiji au mtaa.

*1. Hodi hodi naingia, uwanjani mwaniona,*
*Faida kuzingatia, utunzaji niloona,*
*Hewa safi shangilia, na afya zetu kunona,*
*Tuyatunze mazingira, yatutunze nasi pia.*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 11 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. *Magonjwa mengi epuka, tutunzapo mazingira,*
*Maji mengi tutateka, kwa mazingira imara,*
*Mandhari kusifika, kupendeza na kung'ara,*
*Tuyatunze mazingira, yatutunze nasi pia.*

3. *Rutuba nzuri twapata, tutunzapo mazingira,*
*Mali nyingi tutapata, pasipo hata hasara,*
*Viumbe wengi kupata, maisha kuwa imara,*
*Tuyatunze mazingira, yatutunze nasi pia.*

## Zoezi la 6

1. Je, ni faida gani za utunzaji wa mazingira zilizomo katika shairi ulilolisoma?
2. Taja faida nyingine za utunzaji wa mazingira unazozifahamu.
3. Andika sentensi tano kuelezea faida za utunzaji wa mazingira mtaani au kijijini kwako.

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako kutunga beti mbili za shairi linaloelezea faida za utunzaji wa mazingira katika kijiji au mtaa wenu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 12 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Andika habari fupi kuhusu utunzaji wa mazingira ya kijiji au mtaa wako unavyofanyika.
2. Eleza kwa ufupi utakavyotumia maarifa na stadi ulizopata katika sura hii kwenye maisha yako ya kila siku.
3. Eleza matendo tunayopaswa kuyafanya ili kutunza mazingira yetu.

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi*.

4. Mazingira hutunzwa na wanafunzi tu.____________
5. Majengo, mimea, wanyama na magari ni baadhi ya vitu vinavyounda mazingira.______________
6. Kulima kwa kufuata kanuni bora za kilimo ni mbinu mojawapo ya kutunza mazingira.______________
7. Mifugo mingi katika eneo moja huzuia uharibifu wa mazingira.________________

### Msamiati

| | |
|---|---|
| Gereji: | sehemu ya kufanyia matengenezo na kuhifadhi magari, pikipiki na baiskeli |
| Karakana: | sehemu panapotengenezwa na kuundia vitu |
| Kitongoji: | eneo dogo la makazi ya watu katika kijiji |
| Kozi: | mafunzo ambayo mtu hupewa ili awe na utaalamu juu ya kitu au jambo fulani |
| Mandhari: | muonekano wa eneo fulani maalumu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Matukio ya kihistoria

Katika sura hii, utajifunza matukio yaliyotokea katika familia yako na shuleni. Pia, utajifunza njia za kupata taarifa za matukio. Vilevile, utajifunza vifaa vinavyotumika kuchukua taarifa za matukio. Mwisho, utajifunza njia za kutunza taarifa za matukio ya kihistoria.

### Matukio ya kihistoria katika jamii

Matukio ya kihistoria hutokea kila siku katika maisha. Matukio haya ni kama vile siku ya uhuru na siku ya kifo cha Baba wa Taifa. Pia, siku yako ya kuzaliwa na hata siku ya kuanza shule ni miongoni mwa matukio ya kihistoria.

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.**

Mwalimu wetu wa somo la Maarifa ya Jamii alimwalika mgeni. Mgeni huyo alikuwa anaitwa mzee Kahonda. Mzee Kahonda alikuja kuelezea juu ya matukio yaliyowahi kutokea katika familia yake. Tulijiandaa kumuuliza maswali ili tuweze kuelewa vizuri alichokusudia kutusimulia. Mgeni alikaribishwa na mwalimu darasani ili azungumze nasi. Mazungumzo yalikuwa hivi:

**Mzee Kahonda:** Hamjambo wanafunzi?

**Wanafunzi:** Hatujambo, *s*hikamoo mzee Kahonda.

**Mzee Kahonda:** Marahaba! Mnaendeleaje na masomo?



FOR ONLINE USE ONLY

Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 14 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Wanafunzi:** Tunaendelea vizuri.

**Mzee Kahonda:** Nimealikwa na mwalimu wenu kuja kuelezea matukio yaliyowahi kutokea katika familia yangu. Ninaamini mtajifunza mengi, hivyo nisikilizeni kwa makini. Muwe huru kuuliza maswali. Miaka kumi iliyopita katika familia yangu, palitokea moto mkubwa. Moto huo uliunguza nyumba na vitu vyote vilivyokuwa ndani. Vitu kama vyakula, nguo, madaftari na sare za shule za watoto na wajukuu zangu viliungua. Wanafamilia walilia na kuumia sana.

(*Mzee Kahonda alipomaliza kusimulia alituruhusu tumuulize maswali. Mwanafunzi wa kwanza kuuliza swali alikuwa Halima.)*




**Kielelezo namba 1:** *Wanafunzi wa darasa la nne wakimsikiliza mzee Kahonda*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Halima:** (*Akasimama na kuuliza*). Chanzo cha moto kilikuwa ni nini?

**Mzee Kahonda:** Ilikuwa hitilafu ya umeme.

**Katembu:** Baada ya tukio hilo, hali ilikuwaje?

**Mzee Kahonda:** Hali haikuwa nzuri kwani vitu vyote viliteketea kwa moto. Lakini ndugu na majirani walitusaidia chakula na kutuchangia fedha. Fedha zilitumika kununulia vifaa vya kujengea nyumba yetu upya. Kwa sasa tunaendelea na maisha kama hapo awali.

**Machupa:** Pole sana mzee wetu.

**Mzee Kahonda:** Asante sana. Mbali na tukio la moto, yapo matukio mengine yaliyotokea katika familia yangu.

**Katunda:** Ni yapi hayo?

**Mzee Kahonda:** Mwaka juzi tulikuwa na sherehe za mavuno.

**Runia:** Mlisherehekea mavuno ya nini?

**Mzee Kahonda:** Familia za ukoo wangu huwa na utaratibu wa kusherehekea pale tunapomaliza kuvuna mazao. Mwaka juzi tulivuna magunia mia moja ya mpunga. Wanafamilia walifanya sherehe iliyoambatana na kuimba nyimbo na kucheza ngoma za asili.

**Kagoma:** Ahaa! Sherehe hizi huwa na faida gani kwa wanafamilia?

**Mzee Kahonda:** Sherehe hizi huleta umoja, ushirikiano na mshikamano kwa wanafamilia. Pia,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huongeza hamasa ya kushiriki kufanya kazi kwa msimu ujao wa kilimo. Vilevile, hujenga na kudumisha utamaduni wa familia yetu.

Wanafunzi, yapo matukio mengi yaliyotokea katika familia yangu. Nikipata muda nitakuja tena kuwasimulia. Asanteni kwa kunisikiliza.

**Wanafunzi:** (*Wote kwa pamoja walipiga makofi kwa kumshangilia mzee Kahonda).*

**Mwalimu:** Mgeni wetu tunakushukuru kwa kuja. Wanafunzi, bila shaka mmeelewa matukio yaliyowahi kutokea katika familia kupitia masimulizi ya mgeni wetu. Je, mmefurahia simulizi za mzee Kahonda?

**Wanafunzi:** Ndiyo, tumefurahi sana mwalimu.

**Halima:** Mwalimu, tunaomba umwalike tena mgeni wetu siku nyingine.

**Mwalimu:** Sawa Halima, nitafanya hivyo.

Kuna matukio mengine mengi yanayotokea katika familia nyingi za kitanzania. Baadhi ya matukio hayo ni kama vile sherehe za mavuno na harusi. Matukio mengine ni mashindano ya ngoma za kiutamaduni na misiba ya wanandugu. Familia nyingine hukumbwa na matukio ya nyumba kuvamiwa na majambazi au wizi wa mifugo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, baadhi ya familia husherehekea siku zao za kuzaliwa. Familia nyingine huwafanyia sherehe za harusi vijana wao wanapooa au kuolewa. Kila familia huwa na matukio tofauti na familia nyingine. Tofauti hii hutegemea aina ya tukio na wakati tukio linapotokea. Matukio mengine katika familia hufurahisha na mengine huhuzunisha. Mfano wa tukio la kufurahisha ni harusi na mfano wa tukio la kuhuzunisha ni msiba.

**Zoezi la 1**

1. Ni ujumbe gani umeupata kutokana na simulizi ya mzee Kahonda?
2. Taja matukio mawili yaliyosimuliwa na mzee Kahonda.
3. Je, unakumbuka matukio yaliyowahi kutokea katika familia yako? Ni yapi?
4. Ni wakati gani familia yenu hufanya sherehe?

**Kazi ya kufanya**

Msimulie mwenzako tukio moja la furaha lililowahi kutokea katika familia yako. Unapaswa kusema wakati na nini kilitokea. Andika tukio hilo kwenye daftari lako.

## Matukio ya kihistoria katika Shule ya Msingi Kibeho

Katika Kijiji cha Kitufe kuna shule ya msingi iitwayo Kibeho. Shule ya Msingi Kibeho ilianzishwa mwaka 2008. Shule hii ilijengwa kwa nguvu za wananchi. Wananchi walijenga shule ili kupunguza umbali mrefu waliokuwa wakitembea watoto wao



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwenda shuleni. Shule ya Msingi Kibeho ilifahamika sana kwa kuwa na wanafunzi wenye nidhamu. Pia, shule hii ilijaliwa kuwa na wanafunzi wenye vipaji vya michezo mbalimbali.

Katika miaka michache iliyopita Shule ya Msingi Kibeho ilikuwa maarufu sana. Umaarufu huu ulitokana na matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea katika shule hiyo.

*Jedwali lifuatalo linaonesha matukio yaliyowahi kutokea shuleni Kibeho.*

| **Mwaka** | **Matukio** |
|---|---|
| 2012 | i. Sherehe za Mwenge wa Uhuru kimkoa zilifanyika shuleni.<br>ii. Shule yetu ilitoa mwanafunzi bora kimkoa katika mtihani wa darasa la nne. |
| 2013 | i. Mashindano ya michezo ya kata yalifanyika katika uwanja wa Kibeho. Shule ya Msingi Kibeho ilishinda kombe la mpira wa miguu na mpira wa pete.<br>ii. Uzinduzi wa madarasa matatu mapya. |
| 2014 | i. Sherehe za mahafali ya kwanza ya Darasa la Saba.<br>ii. Sherehe za kuwakaribisha walimu wapya. |
| 2015 | i. Mkuu wa Mkoa alitembelea shule yetu.<br>ii. Sherehe za kuwapongeza wanafunzi bora waliofanya vizuri kitaifa katika mtihani wa Darasa la Saba. |
| 2016 | i. Tulipokea kompyuta mpya kutoka kwa wafadhili.<br>ii. Paa la jengo la Darasa la Nne liliezuliwa na upepo mkali.<br>iii. Ulitokea msiba wa mwanafunzi wa Darasa la Nne. |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 19 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hadi sasa yapo matukio mbalimbali yanayoendelea kutokea katika shule ya Kibeho. Mwaka huu shule imeletewa mwalimu mkuu mwingine aitwaye Kavelo Mapupa. Mwalimu huyu amedhamiria kuendeleza taaluma, michezo na nidhamu ya shule hiyo. Kweli Shule ya Msingi Kibeho imekuwa na mafanikio makubwa.

**Kazi ya kufanya**

Tembelea ofisi ya mwalimu mkuu na ulizia matukio yaliyowahi kutokea hapo shuleni kwenu. Andika matukio hayo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali. Wasimulie wenzako darasani. Usisahau kumshirikisha mwalimu wako.

*Angalia picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 2:** *Wanafunzi wakichukua taarifa za mashindano ya riadha*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 20 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

1. Je, wewe ungekuwa mmojawapo kati ya wanaochukua taarifa ungetumia vifaa gani kurekodi taarifa?
2. Ni vifaa gani unavitumia mara kwa mara kuchukua taarifa za masomo shuleni?

**Kazi ya kufanya**

(a) Uliza wanafamilia juu ya matukio yaliyowahi kutokea katika familia yako. Andika muda na tukio katika daftari lako la kumbukumbu.

(b) Hebu fikiria kiwanda cha kutengeneza nguo kimeungua kwa moto katika mtaa wa jirani na sehemu unayoishi. Jadiliana na wenzako juu ya:

(i) Vifaa unavyoweza kutumia kuchukua taarifa za tukio hilo.

(ii) Ni njia gani watu wengine wanaweza kutumia kupata taarifa za tukio hilo?

(iii) Njia unazoweza kutumia katika kutunza taarifa za tukio hilo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Njia zinazotumika kupata taarifa za matukio

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Umejifunza matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea katika familia na shuleni. Zipo njia mbalimbali za kupata taarifa za matukio hayo. Tunaweza kutumia simulizi, redio na runinga. Wakati mwingine njia kama magazeti, vitabu na simu hutumika kupata taarifa za matukio.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 21 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baadhi ya taarifa za matukio hupatikana kwa njia ya masimulizi au mitandao. Jamii nyingine huwa na sehemu maalumu za kumbukumbu kama makumbusho. Watu wengine hutembelea maktaba na kusoma vitabu na majarida mbalimbali ili kupata taarifa za matukio. Ukifanya uchunguzi kwa kuuliza watu juu ya jambo fulani unaweza pia kupata taarifa za matukio.

Ni vema kutunza taarifa za matukio yanayotokea katika familia zetu na shuleni. Unaweza kuchukua taarifa za matukio kwa kutumia vifaa kama kalamu na daftari. Vifaa hivi hutumika kuandika taarifa za matukio. Wakati mwingine watu hutumia kamera kupiga picha za matukio mbalimbali.

Ni muhimu kutambua kuwa tukio likitokea, huna budi kuchukua taarifa zake na kuzitunza. Hii husaidia kuwa na kumbukumbu za matukio hayo.

**Zoezi la 3**

1. Ni njia gani zilizotajwa katika habari hii unazozitumia mara kwa mara kupata taarifa za matukio?
2. Taja njia tatu nyingine unazoweza kutumia ili kupata taarifa za matukio.
3. Ni vifaa gani utakavyotumia kurekodi taarifa wakati wa kutembelea sehemu maalumu kama vile mbuga za wanyama?
4. Je, kuna umuhimu wa kutafuta taarifa za matukio?

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 22 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutunza kumbukumbu za matukio ya masomo

Unatakiwa kutunza kumbukumbu za matukio yanayotokea shuleni. Matukio mengi yanatokea katika jamii na hata shuleni. Matukio haya yanaweza kuwa ya kihistoria au yasiwe ya kihistoria.

*Angalia mchoro unaoonesha vifaa vya kutunza kumbukumbu za matukio ya masomo shuleni, kisha jibu maswali.*




**Kielelezo namba 3:** *Vifaa vya kutunzia kumbukumbu za matukio ya masomo shuleni*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 23 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Ni ujumbe gani umeupata kutokana na mchoro huo?
2. Taja vitu saba vinavyotumika kutunza kumbukumbu za matukio ya masomo shuleni.

## Umuhimu wa kutunza kumbukumbu

Soma shairi, kisha jibu maswali.

*1. Mbele yenu tokezea, jambo nataka kunena,*
*Ninapenda elezea, kumbukumbu naziona,*
*Zamani yalotokea, hadi sasa twayaona,*
*Kumbukumbu zitunzeni, turejee yalopita.*

*2. Kumbukumbu kuzitunza, ni muhimu nawambia,*
*Historia twajifunza, kumbukumbu zatwambia,*
*Habari tukizitunza, hazina kuhifadhia,*
*Kumbukumbu zitunzeni, turejee yalopita.*

*3. Kutotunza kumbukumbu, mambo mengi hupotea,*
*Asotunza kumbukumbu, hukosa la kunenea,*
*Kutotunza kumbukumbu, hasara hututokea,*
*Kumbukumbu zitunzeni, turejee yalopita.*

*4. Kuzitunza kumbukumbu, tabia njema jengea,*
*Ukiwa na kumbukumbu, heshima kujiwekea,*
*Jiwekee kumbukumbu, kwa yale yalotokea,*
*Kumbukumbu zitunzeni, turejee yalopita.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Ni ujumbe gani umeupata kutoka kwenye shairi ulilosoma?
2. Ni faida zipi za kutunza kumbukumbu za masomo shuleni zilizotajwa kwenye shairi?
3. Taja vifaa vinne vya kutunza kumbukumbu za masomo yako shuleni.
4. Ni vifaa vipi unatumia kutunza kumbukumbu za matukio nyumbani kwenu?
5. Nini kitatokea usipotunza kumbukumbu za masomo yako?

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Eleza kwa kifupi utatumiaje maarifa uliyoyapata katika sura hii.
2. Taja vifaa vitano vinavyotumika kunakili taarifa za matukio mbalimbali.
3. Eleza namna unavyotunza kumbukumbu za masomo yako shuleni.
4. Elezea jinsi utakavyowashauri wanafunzi wenzako juu ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu.
5. Eleza umuhimu wa kupata habari za matukio mbalimbali.

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

6. Unaweza kuchukua nukuu za matukio kwa kutumia daftari na kalamu. _________
7. Hakuna umuhimu wa kutunza kumbukumbu za matukio yanayotokea katika familia. ________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Taarifa za matukio zinaweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya hadithi. ___________
9. Makumbusho ni sehemu ambayo kumbukumbu mbalimbali za kihistoria huhifadhiwa.______________
10. Mkoba, kabati na mfuko wa shule ni vifaa vinavyotumika kutunza kumbukumbu. _________________

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Hamasa: | msukumo wa ndani wa kufanya jambo |
| Hitilafu: | kasoro katika utendaji |
| Kunena: | kusema jambo |
| Kurekodi: | kuchukua au kuandika taarifa kwa kalamu kwenye karatasi au kwa njia ya kielektroniki ili kuisoma au kujikumbusha baadaye |
| Maktaba: | nyumba au chumba ambacho hutumika kuhifadhi na kusomea machapisho au vitabu |
| Simulizi: | hadithi za matukio halisi au za kubuni zinazohusu hali halisi ya maisha |
| Ukoo: | muunganiko wa familia nyingi zenye asili moja |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Hali ya hewa

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza dhana ya jotoridi, dalili za hali ya joto na baridi. Pia, ulijifunza kupima jotoridi, kusoma vipimo vyake na kuelezea hali ya jotoridi ya eneo. Vilevile, ulibainisha njia za kujikinga na hali ya hewa ya baridi na joto katika mazingira. Katika sura hii, utajifunza dhana ya hali ya hewa na kipengele cha hali ya mvua. Pia, utajifunza dhana ya mabadiliko ya hali ya hewa. Utajifunza madhara yatokanayo na mvua kubwa na namna ya kujikinga.

FOR ONLINE USE ONLY

### Dhana ya hali ya hewa

Kila siku kuna hali ya hewa fulani ambayo hutawala katika mazingira yetu. Hali ya hewa inajumuisha vipengele kama upepo, mvua na halijoto. Pia, hujumuisha hali ya mawingu, unyevuanga, mgandamizo wa hewa na mwanga wa jua. Hali ya hewa hurekodiwa kwa muda mfupi. Mara nyingi hurekodiwa kwa saa au kwa siku. Hali ya hewa hurekodiwa katika kituo cha kurekodi hali ya hewa. Kila kipengele cha hali ya hewa hupimwa kwa kifaa maalumu.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 27 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali.*

Baromita



Mimi naitwa **MGANDAMIZO WA HEWA.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **BAROMITA.** Kipimio changu ni **Milibaa.**

Kipimajoto




Mimi naitwa **JOTORIDI.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **KIPIMAJOTO.** Kipimio changu ni **Kizio cha Sentigredi au Farinaiti.**

**VIPENGELE VYA HALI YA HEWA**

Kipimamvua



Mimi naitwa **MVUA.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **KIPIMAMVUA.** Kipimio changu ni **Milimita.**

Kipimaupepo




Anemomita



Mimi naitwa **UPEPO.** Ninapimwa kwa vifaa viitwavyo **KIPIMAUPEPO** na **ANEMOMITA.** (Kipimaupepo kinapima mwelekeo wa upepo na Anemomita inapima kasi ya upepo). Vipimio vyangu ni **Kilomita kwa Saa** na **Kizio cha uelekeo**.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 28 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mimi naitwa **MAWINGU.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **KIPIMAMAWINGU.** Kipimio changu ni **Okitasi.**

**VIPENGELE VYA HALI YA HEWA**

Haigromita




Mimi naitwa **UNYEVUANGA.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **HAIGROMITA.** Kipimio changu ni **Asilimia.**

Kampbeli Stoki



Mimi naitwa **MWANGA WA JUA.** Ninapimwa na kifaa kiitwacho **Kampbeli Stoki.** Kipimio changu ni **Saa**

**Kielelezo namba 1:** *Vipengele vya hali ya hewa na vifaa vya kupimia kila kipengele*

## Zoezi la 1

1. Eleza hali ya hewa inavyokuwa mara kwa mara katika eneo unaloishi.
2. Taja vifaa vinavyotumika kupima vipengele vifuatavyo vya hali ya hewa.
   (a) jotoridi (b) mvua (c) unyevuanga
   (d) mgandamizo wa hewa.
3. Chora vifaa vifuatavyo:
   (a) Kipimajoto (b) Anemomita (c) Kipimamvua
4. Joto la binadamu hupimwa kwa kutumia kifaa gani?
5. Sehemu ambapo hali ya hewa inarekodiwa panaitwaje?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 29 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Chunguza hali ya hewa unapoamka alfajiri, je, unahisi hali gani ya hewa? Je, ni baridi kali, joto kiasi au joto kali? Chunguza anga siku ya leo. Je, anga linaonekanaje? Je, limefunikwa na mawingu au la? Je, wakati wa mchana hali ikoje? Chunguza wakati wa jioni na usiku. Je, hali huendelea kuwa ileile au hubadilika? Andika taarifa kwenye daftari lako, kisha wasimulie wenzako.

## Mabadiliko ya hali ya hewa

Mabadiliko ya hali ya hewa ni ile hali ya kubadilika kwa vipengele vya hali ya hewa. Wakati fulani anga linaweza lisiwe na mawingu na jotoridi likawa juu. Baada ya muda mfupi, anga likafunikwa na mawingu na jotoridi likashuka. Kasi ya upepo inaweza ikaongezeka. Mvua kubwa pia huweza kunyesha. Baada ya muda kidogo mvua huacha kunyesha na ghafla anga likawa jeupe tena.

Hali hii huitwa mabadiliko ya hali ya hewa. Hata hivyo, si kila siku kila kipengele cha hali ya hewa hutokea. Kuna siku inaweza kupita bila mvua kunyesha au joto kuongezeka.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 30 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.**

Fakina na Abdul ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwendokasi iliyopo katika Kijiji cha Bukene. Kijiji hicho hupata mvua mara nyingi. Kijiji cha Bukene kimezungukwa na Ziwa Buke, mito na msitu mnene. Wakati wa jioni, Fakina na Abdul hupendelea kufanya mazoezi katika uwanja uliopo karibu na nyumbani.

Siku moja, Fakina na Abdul walikwenda uwanjani na vifaa vyao vya michezo. Ghafla Fakina alihisi hali ya hewa imeanza kubadilika. Dalili kadhaa za mvua zilianza kuonekana. Dalili hizo ni pamoja na joto kupungua na mwanga wa jua kufifia. Taratibu Fakina aliinua kichwa chake kutazama juu. Lo! Anga lote lilikuwa limefunikwa na mawingu mazito.

Kwa upande mmoja, mawingu yalibadilika na kuwa meusi na kijivu. Ngurumo za radi zilianza kusikika kutokea upande wa Mashariki. Upepo nao uliongeza kasi kutoka upande mvua inakotokea. Ama kweli! Hizi zilikuwa dalili dhahiri za mvua. Fakina alisema, “Abdul rafiki yangu hii mvua iko karibu kunyesha. Hatuna budi kurudi nyumbani”.

Wote walikubaliana kuondoka na walikimbia hadi nyumbani. Fakina alipofika nyumbani alianua mazao na kuingiza mifugo ndani. Abdul naye alianua nguo na kutoa ndoo nje ili kukinga maji ya mvua. Baada ya muda kidogo, upepo uliongezeka huku mwanga wa radi ukionekana na ngurumo zikiendelea kusikika. Punde si punde, mvua kubwa ilinyesha. Ama kweli! Dalili ya mvua ni mawingu, alijisemea Fakina.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuwa na faida katika mazingira. Mvua ikinyesha, husaidia ardhi kupata maji na mimea kukua. Pia, mvua ikinyesha husaidia kurekebisha kiasi cha jotoridi. Vilevile, hutupatia maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na viwandani. Pia, ni chanzo cha maji katika mito, maziwa na bahari. Mvua ni muhimu kwa viumbe hai wanaoishi kwenye maji na nchi kavu.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuwa na madhara mbalimbali. Madhara hayo ni kama mafuriko, kimbunga na radi. Vilevile, husababisha kuzaliana kwa vimelea vya magonjwa mbalimbali katika mazingira yetu. Magonjwa haya ni kama vile homa ya matumbo na kipindupindu. Aidha, huweza kuleta madhara yanayoweza kusababisha vifo, uharibifu wa mali na sura ya nchi.

**Kazi ya kufanya**

1. Nenda nje ya darasa, kisha chunguza hali ya hewa kama kuna upepo, mvua, joto au unyevunyevu. Waelezee wanafunzi wenzako ulichogundua.
2. Wasimulie wenzako darasani hali ya mvua katika maeneo unayoishi ukizingatia:
   (a) Miezi yenye mvua.
   (b) Miezi isiyokuwa na mvua.
   (c) Dalili za mvua.
   (d) Jinsi mnavyotumia mvua katika maeneo unayoishi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 32 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

1. Umejifunza nini katika hadithi hii?
2. Taja dalili nne za mvua zilizotajwa katika hadithi uliyosoma.
3. Abdul alifanya nini kabla ya mvua kuanza kunyesha?
4. Je, kwa nini Fakina alisema dalili ya mvua ni mawingu?
5. Unadhani ni kwa nini Kijiji cha Bukene hupata mvua mara nyingi?
6. Taja faida tatu nyingine za mvua ambazo hazikutajwa kwenye habari uliyosoma.
7. Eleza jinsi utakavyotambua mawingu yenye kuleta mvua.
8. Taja matumizi matano ya maji kwa shughuli za nyumbani.

*Tazama picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 2:** *Madhara yaletwayo na mvua*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Ni madhara gani yaliyosababishwa na mvua kubwa kama ulivyoona katika picha?
2. Taja madhara mengine ambayo hutokea mtaani/kijijini kwako pale mvua kubwa inaponyesha.

**Kazi ya kufanya**

Hebu fikiria rafiki yako anaishi sehemu zenye mvua nyingi. Siku moja anakualika kwenda kumtembelea nyumbani kwao:

(a) Andika kwa ufupi tahadhari utakazochukua kabla ya kwenda kumtembelea rafiki yako.

(b) Ni mambo gani utaulizia kuhusu hali ya hewa kabla ya kwenda?

## Kujikinga na mvua

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Mvua zinaponyesha, huleta faida kwa mimea na wanyama. Wakati mwingine, mvua huambatana na baridi kali, radi na upepo. Hali hiyo, inaweza kuathiri afya ya binadamu na wanyama. Hivyo, mwanadamu anashauriwa kuvaa nguo nzito za kujikinga na baridi. Sweta, jaketi na mgolole huvaliwa wakati wa baridi.

Mvua kubwa huleta madhara makubwa pia. Kucheza kwenye mvua ni hatari kwa afya zetu. Sote tunapaswa kujikinga na mvua kwa kukaa sehemu zisizovuja na zilizo salama. Ili kujikinga na

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 34 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mvua tukae ndani ya nyumba na vibanda. Tunashauriwa tusikae au kusimama chini ya miti wakati wa mvua. Kwa kufanya hivyo tutaepuka madhara yatokanayo na radi. Hii ni kwa sababu, miti mibichi huweza kupitisha umeme wa radi ambao huweza kutudhuru.

Wakati mwingine unaweza ukalazimika kuendelea na shughuli zako huku mvua ikinyesha. Ili kufanya hivyo, unapaswa kuvaa koti la mvua. Koti la mvua haliruhusu maji kupenya. Pia, kutumia mwavuli unapotembea wakati wa mvua. Unashauriwa pia kuvaa viatu visivyoruhusu maji kupenya. Katika sehemu zilizo na mvua nyingi, unashauriwa usiishi karibu na mabonde. Hii ni kwa sababu mabonde ni rahisi kujaa maji na kusababisha mafuriko. Hivyo, inashauriwa kujenga nyumba imara katika maeneo ya mwinuko.

## Zoezi la 4

1. Kutokana na habari uliyosoma, ni vifaa gani hutumika kujikinga na mvua?
2. Taja vifaa vinne vinavyotumika kujikinga na mvua katika mazingira yako.

### Kazi ya kufanya

Chunguza mazingira kutoka shuleni hadi nyumbani. Kisha bainisha sehemu salama za kujikinga na mvua na wasimulie wenzako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 35 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Nini maana ya hali ya hewa?
2. Elezea maana ya mabadiliko ya hali ya hewa.
3. Ni madhara gani ya mvua kubwa uliwahi kushuhudia au kusikia?
4. Eleza namna utakavyojikinga na madhara ya mvua kubwa.
5. Taja dalili tano za mvua unazozifahamu.
6. Kama ungekuwa unaishi sehemu zenye mvua kubwa, ni tahadhari gani ungechukua?

*Oanisha maneno yaliyo katika* **safu A** *na yale ya* **safu B** *ili yalete maana sahihi.*

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 7. Faida ya mvua kwa mimea na binadamu________<br>8. Dalili za mvua__________<br>9. Mawingu yenye kuleta mvua____________<br>10. Mgandamizo wa hewa ________<br>11. Kilimo cha wakati wote__<br>12. Chanzo kikuu cha mito, maziwa na bahari_______ | (a) Baromita<br>(b) mvua za mara nyingi<br>(c) mawingu meusi,mwanga hafifu, ngurumo na radi<br>(d) mvua<br>(e) kupata maji na kukuza mazao<br>(f) mawingu meusi au kijivu<br>(g) ngurumo za radi na mawingu mekundu<br>(h) Anemomita |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 36 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

13. Wakati unafanya kazi kwenye mvua unapaswa kuvaa koti la mvua na kutumia mwamvuli. _______________
14. Namna mojawapo ya kujikinga na madhara ya mvua ni kukata miti yote.__________________
15. Vipengele vinne vya hali ya hewa ni mvua, jua, upepo na mawingu.__________________
16. Uharibifu wa mali na vifo kwa viumbe ni matokeo ya athari za mvua kubwa. _______________
17. Kifaa kinachotumika kupima mvua huitwa Baromita.____

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Anga: | nafasi wazi iliyopo juu ya uso wa Dunia |
| Dhahiri: | onekana wazi, bainika kwa wengi |
| Hali ya hewa: | majumuisho ya hali ya mvua, jotoridi, unyevuanga, upepo na mgandamizo wa hewa |
| Mimea: | kiumbe chenye uhai ambacho kina majani, mizizi, shina, kinachoota kwa kupanda mbegu, mche au tawi |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 37 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Utamaduni wetu

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza matendo ya kusalimiana ya makabila mbalimbali ya kitanzania. Ulijifunza pia kuimba na huku ukicheza michezo ya kiutamaduni inayofahamika. Katika sura hii, utajifunza mambo yanayojenga ushirikiano baina ya watu katika jamii. Aidha, utajifunza mambo yanayosababisha watu kushirikiana katika jamii za Tanzania kwa sasa.

### Ushirikiano baina ya watu katika jamii

Bila shaka huwa unashirikiana na wanafunzi wenzako shuleni katika michezo, kusoma na kufanya usafi. Katika jamii, watu hushirikiana kwenye mambo ya furaha kama harusi na ya huzuni kama vile msiba. Ni vema kutambua kuwa jamii nyingi hupenda kushirikiana katika mambo mbalimbali.

*Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 38 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

b.



c.



**Kielelezo namba 1:** *Matendo yanayoonesha ushirikiano*

## Zoezi la 1

1. Taja mambo yaliyooneshwa katika picha hizi?
2. Kati ya matendo hayo, yapi unaweza kuyafanya?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 39 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mambo yanayojenga ushirikiano katika jamii**

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali.*

**Omari:** Habari yako Ana.

**Ana:** Nzuri Omari, unaendeleaje?

**Omari:** Naendelea vizuri. Naomba kujua mambo yanayojenga ushirikiano katika jamii yetu.

**Ana:** Aah! Omari! Ngoja tujadiliane kwa pamoja.

**Omari:** Sawa! Kuna mambo mengi yanayojenga ushirikiano. Mambo hayo hutofautiana kati ya jamii na jamii.

**Ana:** Ooh! Tuangalie jamii inayotuzunguka Omari.

**Omari:** Katika jamii yetu, watu hushirikiana katika shida na raha. Hushirikiana katika kazi kama vile kilimo, uvuvi na biashara. Pia, hushirikiana kwenye ugonjwa, sherehe na msiba.

**Ana:** Siyo hivyo tu, vilevile watu hushirikiana kwenye ujenzi wa shule na usafi wa mazingira. Pia, husaidiana katika majanga kama mafuriko na moto, na katika utengenezaji wa barabara.

**Omari:** Tunatakiwa tuwajengee watoto wetu ushirikiano toka wakiwa wadogo, ili kuwajengea moyo wa udugu kati yao.

**Ana:** Ama kweli! Inatakiwa wazazi waoneshe ushirikiano huo wakiwa nyumbani na kazini ili watoto wajifunze kwao.

**Omari:** Umesema kweli. Ushirikiano unatakiwa kujengwa kuanzia ngazi ya familia, kisha ukoo, mtaa au kijiji, kata, wilaya, mkoa hadi taifa.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 40 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ana:** Nimekuelewa Omari. Tujitahidi kwa pamoja kujenga ushirikano kwa faida yetu sote. Kwani tukishirikiana tutajenga jamii na taifa lililo imara.

## Zoezi la 2

1. Taja mambo matatu yanayojenga ushirikiano uliyoyasoma katika mazungumzo.
2. Mambo gani mengine hujenga ushirikiano katika jamii yako?
3. Taja matendo matatu ambayo huwa unashirikiana na wenzako shuleni.
4. Ni matendo gani ya furaha ambayo jamii za kitanzania hushirikiana?
5. Je, ni matendo gani ya huzuni ambayo jamii za kitanzania hushirikiana?
6. Andika katika daftari lako faida tano za kushirikiana na wenzako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kuthamini mambo yanayoweza kudumisha ushirikiano katika jamii**

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

Kijiji cha Changarawe kinasifika kwa ushirikiano baina ya wanakijiji. Watu hao hushirikiana katika mambo mbalimbali. Mambo hayo ni kama vile misiba, harusi, majanga ya moto, mafuriko na kimbunga. Mambo mengine ni kilimo, ngoma za asili, jando na unyago.

Siku moja wakati wa msimu wa mavuno, kijiji chetu kilipata msiba mkubwa wa kushtua. Msiba huo ulikuwa wa kifo cha mzee Makopo. Mzee huyo alikuwa maarufu sana na mwenye mashamba makubwa hapo kijijini. Mwenyekiti wa kijiji alipita kutoa tangazo la msiba kwa kila kitongoji. Aliwataka watu wafike msibani ili waweze kutoa michango ya hali na mali. Michango kama vile kuni, unga, mchele na rambirambi ilitolewa.

Akina mama walijitokeza kwa wingi kusaidia shughuli za kupika. Wakati huohuo, kina baba na vijana walishirikiana kuchimba kaburi. Muda wa kuzika ulipofika waliuchukua mwili wa marehemu na kwenda kuuzika. Wanakijiji wote walionesha ushirikiano katika msiba ule. Familia ya mzee Makopo iliwashukuru wanakijiji kwa ushirikiano waliouonesha. Baada ya hapo, watu wote walirudi nyumbani na wengine walibaki na wafiwa. Baada ya siku kadhaa kupita, watu waliendelea na shughuli zao za kawaida.

Shughuli hizo ni pamoja na kuvuna mazao. Baada ya mavuno, wanakijiji walikuwa na desturi ya kusherehekea mavuno yao.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 42 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika sherehe hizo watu walikula, kunywa, kuimba na kucheza nyimbo za asili.

Pia, watu wa Changarawe husalimiana na kuzungumza lugha yao ya asili ili kukuza utamaduni wa jamii yao. Mambo mengine yaliyoweza kudumisha ushirikiano katika jamii hiyo, ni kuwa wakweli, wachapakazi, wawazi na waadilifu. Jamii nyingi zina mfumo wa maisha unaokaribiana na ule wa wakazi wa Changarawe. Kwa hakika tudumishe utamaduni wetu ili tuweze kushirikiana na kusaidiana katika jamii zetu.

**Zoezi la 3**

1. Andika kichwa cha habari uliyosoma.
2. Habari hii inakufundisha nini?
3. Ni vitendo gani vilivyoonesha ushirikiano baina ya wakazi wa Changarawe?
4. Taja mambo manne uliyojifunza katika habari hii.
5. Familia yako hushirikiana na familia nyingine katika mambo gani?

## Kuvunjika kwa ushirikiano

Kama tulivyoona hapo awali, jamii nyingi hushirikiana katika mambo mbalimbali. Tumeona kwamba, watu hushirikiana katika misiba na harusi. Pia, hushirikiana katika sherehe za mavuno, ngoma za utamaduni na mambo mengine mengi. Vilevile, shuleni tunashirikiana na marafiki zetu katika mambo mbalimbali. Fikiria kuwa umekuwa na ushirikiano na rafiki yako katika masomo shuleni. Siku moja, unagundua kwamba rafiki yako anaonesha tabia zifuatazo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Ubinafsi na uchoyo kwa vitu vyake. Hapendi kukugawia wewe wala rafiki zake wengine kitu chake.
(b) Anatoa siri zako kwa wanafunzi wengine.
(c) Anaonekana mtu mwema kwako lakini anakusema vibaya kwa wengine.
(d) Ukifaulu mtihani, anachukia.
(e) Anakuonea wivu akiona umenunua vitu vipya.
(f) Anaonesha tabia za udokozi.
(g) Anakuwa mtoro shuleni.
(h) Anakuwa mvivu katika kazi.

Ukigundua rafiki yako ana tabia hizo, bila shaka ushirikiano wenu utavunjika. Pia, hata katika jamii za watu ambako wanashirikiana vizuri, wakati mwingine ushirikiano huvunjika. Hii inaweza kusababishwa na mtu kuwa mchoyo au mbinafsi. Vilevile, husababisha kutoshirikiana na wenzake katika matukio mbalimbali, au kuwa na tabia za wizi. Matendo haya si ya kuigwa kwa sababu huvunja ushirikiano.

## Zoezi la 4

1. Utatumiaje ujumbe ulioupata katika sura hii katika maisha yako ya kila siku?
2. Taja sababu tatu zinazoweza kuvunja ushirikiano wako na wenzako.
3. Taja sababu nne zinazoweza kusababisha watu kutoshiriki shughuli za kijamii katika mtaa au kijiji chenu.
4. Utawashaurije marafiki ambao ushirikiano wao umevunjika?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya

Chunguza wanafunzi ambao walikuwa na ushirikiano kisha ukavunjika. Toa sababu zilizosababisha kuvunjika kwa ushirikiano huo. Andika uchunguzi huu daftarini, kisha wasimulie wenzako darasani.

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Eleza mambo uliyojifunza katika sura hii.
2. Eleza namna unavyoweza kuhamasisha familia yako kushirikiana na majirani zenu.
3. Taja sababu tatu za kudumisha utamaduni wetu.
4. Orodhesha hasara mbili tutakazopata tusipodumisha utamaduni.
5. Taja mambo ambayo yanafanya watu wadumishe ushirikiano.

Andika **NDIYO** kama sentensi ni sahihi na **HAPANA** kama sentensi si sahihi.

6. Watu hushirikiana katika matendo ya misiba, harusi, sherehe za mavuno na ngoma.____________
7. Kuzungumza lugha ya asili hukuza utamaduni wetu.______
8. Ni lazima ushirikiane na kila mtu katika jamii.____________
9. Uhusiano ni matokeo ya ushirikiano._______________
10. Siyo lazima watu washirikiane kwa kila tukio linalotokea katika jamii. ______________

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 45 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Desturi: | mambo ya mazoea yanayotendwa kila siku na jamii |
| Jando: | utaratibu wa kuwatahiri watoto wa kiume na kuwapatia mafunzo kuhusu maisha |
| Janga: | tukio la hatari ambalo husababisha maafa au balaa |
| Unyago: | mafunzo ya nadharia na vitendo yanayohusu malezi kwa wavulana na wasichana kuhusu mila na desturi za jamii zao, yanayojumuisha ngoma na nyimbo |
| Ushirikiano: | hali ya watu kuungana na kufanya jambo fulani kwa pamoja |
| Utamaduni: | mwenendo wa maisha unaohusisha asili, mila, desturi, jadi au itikadi inayotawala katika jamii fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Uhusiano mwema katika jamii

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza chimbuko la familia. Pia, uhusiano wa watu katika familia na marafiki. Vilevile, ulijifunza faida za kuwa na uhusiano mwema kati ya marafiki shuleni. Hali kadhalika, ulijifunza hasara za kutokuwa na uhusiano mwema na marafiki. Katika sura hii, utajifunza dhana ya uhusiano na chimbuko la ukoo. Pia, utajifunza jamii za kale za Ujima na Ukabaila.

### Maana ya uhusiano

Uhusiano ni hali ya kuwa na mfungamano wa kindugu au kirafiki katika mambo mbalimbali. Uhusiano unaweza kuwa kati ya mtu na mtu, kundi la watu katika jamii au taifa moja na jingine.

### Uhusiano mwema

Ushirikiano wa watu katika shughuli mbalimbali hujenga uhusiano mwema. Watu wakiwa na uhusiano mwema husaidiana, hupendana na huheshimiana. Ili kuishi vizuri katika jamii, ni vema ukawa na uhusiano mwema na wenzako. Uhusiano mwema unaweza kujengwa tunapokuwa nyumbani, shuleni au mahali popote katika jamii. Uhusiano mwema haubagui jinsia, kabila, umri, dini wala rangi. Uhusiano mwema huleta mafanikio. Kwa hiyo, ni vizuri kuwa na uhusiano mwema na watu wote.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 47 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



b.





Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 48 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

c.



**Kielelezo namba 1:** *Matendo ya uhusiano katika shughuli mbalimbali*

## Zoezi la 1

1. Taja matendo matatu yanayoonesha uhusiano mwema katika picha.
2. Je, una uhusiano mzuri na wanafunzi wenzako? Huwa unafanya nini kuonesha uhusiano huo?
3. Taja matendo mengine mawili yanayoonesha uhusiano mwema katika darasa lako.
4. Andika matendo manne yanayoonesha uhusiano mwema katika mtaa au kijiji chako.

### Kazi ya kufanya

Jadiliana na wenzako mambo yanayoonesha uhusiano mwema katika familia zenu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhusiano katika familia

*Soma mazungumzo, kisha jibu maswali.*

**Sekeke**: Habari yako Kibonge.

**Kibonge:** Nzuri.

**Sekeke:** Loo! Mbona nakuona kama unafanya kazi nyingi sana nyumbani kwenu?

**Kibonge:** Hapana Sekeke, kila mmoja wetu anafanya kazi alizopangiwa.

**Sekeke:** Ahaa! Kwetu pia tuna utaratibu wa kusaidiana kazi. Mimi nafanya kazi za kuosha vyombo, kufua na kupika chakula.

**Kibonge:** Hata kwetu kila mwanafamilia hutimiza wajibu wake kwa wakati. Sisi watoto kwa mfano hutimiza wajibu wetu wa kusafisha nyumba. Pia, hulima bustani za mboga, kufua na kuosha vyombo bila kusimamiwa.

**Sekeke:** Vilevile, kwenye familia yetu tunapendana sana. Tunafanya sherehe za kuzaliwa na wazazi hutupeleka sehemu nzuri kupunga upepo.

**Kibonge:** Sisi tunamjali kila mmoja bila kubagua. Mimi nikirudi kutoka shuleni, nambeba mdogo wangu na kucheza naye. Baba akirudi kutoka kazini, hutuletea zawadi. Pia, hutuuliza kama tumekula na kuoga.

**Sekeke:** Ooh! Kumbe kweli mnaishi vizuri. Hata kwenye familia yetu tunaheshimiana sana. Tunapoamka tunawasalimu wazazi. Mimi pia, huwasalimu dada na kaka.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 50 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kibonge:** Vizuri sana, hiyo ni heshima kubwa kwa wanafamilia. Sifa kubwa kwetu sisi ni kutokugombana. Haijawahi kutokea wanafamilia wakagombana. Kwani tunashirikiana, tuna amani na furaha siku zote.

**Sekeke:** Vizuri Kibonge! Nimejifunza kwamba upendo na umoja ni mambo ya msingi katika familia. Tufanye kazi zetu kwa pamoja kama vile kulima, kupika, kuosha vyombo na kulisha mifugo.

**Kibonge:** Sawa Sekeke. Pia, tukumbuke kwamba amani na utulivu ndiyo nguzo katika familia. Familia yenye amani na utulivu, hujenga mahusiano yaliyo thabiti, hivyo hupata maendeleo.

## Zoezi la 2

1. Je, umejifunza nini kutokana na mazungumzo uliyoyasoma?
2. Taja faida nne nyingine za uhusiano mwema ambazo hazikutajwa katika habari hii.
3. Orodhesha hasara tatu za kutokuwa na uhusiano mzuri shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 51 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Faida za uhusiano katika familia**

Soma wimbo, kisha jibu maswali.

1. *Ni uhusiano mwema, uwanjani naingia,*
*Nipokeeni kwa wema, na faida zake pia,*
*Tuhusiane kivyema, upendo kudumishia,*
*Uhusiano jamani, hujenga jamii bora.x2*

2. *Muhimu tuhusiane, tujenge mshikamano,*
*Ni vizuri tupendane, kujenga uhusiano,*
*Mazuri elimishane, kukuza mahusiano,*
*Uhusiano jamani, hujenga jamii bora.x2*

3. *Uhusiano jamani, marafiki ongezeka,*
*Umoja pia amani, nguvu pia kujengeka,*
*Upendo ule wa ndani, uhusiano sabika,*
*Uhusiano jamani, hujenga jamii bora.x2*

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 3**

1. Umejifunza nini kutokana na wimbo huu?
2. Ni faida gani utazipata ukiwa na uhusiano mwema na wenzako?
3. Unafikiri nini kitatokea tusipojenga uhusiano mwema na wenzetu?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 52 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhusiano katika jamii

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

Siku moja, Rehema na Halima waligombana wakiwa shuleni. Rehema aliporudi nyumbani alikwenda kisimani kuchota maji. Huko alikutana na Halima. Rehema alichota maji na kumuomba Halima amsaidie kumtwisha ndoo. Halima alikataa kwa kumuangalia tu bila kujibu chochote.

Rehema alipojaribu kujitwisha ndoo, ghafla ilianguka puu! Maji yote yalimwagika. Ndoo nayo ilipasuka. Rehema alikasirika sana, alirudi nyumbani bila maji. Alipofika nyumbani mama yake alimuuliza Rehema, "Maji yapo wapi?" Rehema alijibu, "Mama! Ndoo imepasuka, nilimuomba Halima anitwishe lakini alikataa. Ndoo ilianguka, ikapasuka na maji yalimwagika."

Mama alimuuliza, "Kwa nini alikataa kukutwisha?" Rehema alimjibu, "Tuligombana shuleni." Mama yake alimwambia, "Mimi na baba yako tumekuwa tukikusihi usigombane na watu. Kuwa na uhusiano mwema na watu wote. Ukigombana na watu utakosa msaada pale unapohitaji. Pia, utakosa furaha, amani, upendo pamoja na ushirikiano na wenzako." Mama yake alimkanya asirudie tena kugombana.

### Zoezi la 4

1. Kwa nini Halima alikataa kumtwisha Rehema ndoo?
2. Rehema aliambiwa nini na wazazi wake?
3. Kwa nini ni jambo jema kusaidiana unapokuwa nyumbani au shuleni?
4. Taja madhara manne utakayoyapata kwa kutokuwa na uhusiano mwema na wenzako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 53 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ukoo wetu

Bila shaka wewe umetoka katika ukoo fulani. Kila mtu anatokea ukoo fulani. Ukoo ni muunganiko wa familia zenye asili au chimbuko la aina moja.

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.**

Mimi ninasoma Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Mshikamano. Mwalimu wetu wa darasa anaitwa Furaha. Siku moja mwalimu Furaha alitusimulia habari za mzee Kingu. Mwalimu Furaha alituambia kuwa mzee Kingu anajua habari za koo mbalimbali hapa kijijini kwetu. Siku moja atamwalika aje kutusimulia habari za ukoo na namna unavyokuwa au kuongezeka. Siku iliyofuata, ilikuwa siku ya somo la Maarifa ya Jamii. Mwalimu Furaha alimwalika mzee Kingu aje darasani kwetu.

FOR ONLINE USE ONLY

Mazungumzo kati ya mwalimu Furaha, mzee Kingu na wanafunzi yalikuwa kama ifuatavyo:

**Mwalimu Furaha:** Shikamoo mzee Kingu!

**Mzee Kingu:** Marahaba mwalimu Furaha.

**Mwalimu Furaha:** Karibu mzee Kingu uelezee habari ya ukoo wako kwa wanafunzi. Wanafunzi watasikiliza kisha wataenda kuchunguza habari za koo zao kisha watasimulia darasani.

**Mzee Kingu:** Asante mwalimu. Hamjambo wajukuu zangu?

**Wanafunzi:** Hatujambo! shikamoo babu!

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mzee Kingu:** Marahaba wajukuu zangu. Mimi ni mtoto wa kwanza kuzaliwa kwa mzee Rushashele. Mama yangu ni bibi Hedaya. Tulizaliwa watoto watatu wa kiume. Majina yetu ni Kingu, Kamleti na Kipala. Mimi nimemuoa Zena, Kamleti kamuoa Dengua. Kipala naye kamuoa Dumeka. Kwa hiyo nina shemeji wawili. Baba na mama yangu wana wakwe watatu ambao ni Dumeka, Zena na Dengua. Mimi pamoja na wote niliowataja ni wanaukoo.

**Wanafunzi:** Ukoo wenu unaitwaje?

**Mzee Kingu:** Ukoo wetu unaitwa ukoo wa Rushashele.

**Wanafunzi :** Je, wewe na ndugu zako mna familia zenu?

**Mzee Kingu:** Ndiyo! Mimi na ndugu zangu tunazo familia zetu. Tena tumezaa watoto. Mimi na Zena tulizaa watoto watatu. Wanaitwa Zebedayo, Hamisa na Karomo. Hamisa aliolewa na Hatibu. Hamisa na Hatibu walizaa watoto wawili. Watoto hao ni wajukuu zangu ambao pia ni vitukuu vya mzee Rushashele. Kamleti alizaa mtoto mmoja aitwaye Hadija. Kipala na Dumeka walizaa watoto watatu. Majina yao ni Otamu, Odula na Hamidu. Hamidu alizaa watoto wawili. Watoto hao ni Edomi na Etausi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa kutumia mti wa ukoo wa mzee Kingu utajifunza namna wanaukoo wanavyohusiana katika jamii.




**Kielelezo namba 2:** *Mti wa ukoo*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Chimbuko la ukoo ni nini?
2. Watoto wangapi walizaliwa na Hamidu na Siane? Taja majina yao.
3. Hadija atamuitaje mzee Rushashele?
4. Watoto waliozaliwa na Otamu na Zebena wanaitwaje?
5. Ukoo wa mzee Rushashele una idadi ya familia ngapi?

**Kazi ya kufanya**

Waulize wazazi au walezi wako, je, wewe ni mjukuu na kitukuu wa nani katika familia yenu?

## Migogoro katika ukoo

Soma wimbo, kisha jibu maswali.

1. *Jamani ndugu zanguni, uonevu ulozidi,*
*Sisi ukoo wa Mbuni, migogoro imezidi,*
*Migogoro ardhini, ugomvi umezidi,*
*Migogoro tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

2. *Kurithi mali za kwetu, wanaume wapombele,*
*Wakike hakuna kitu, mambo kutokuwa mbele,*
*Watoto pasipo kitu, kisa ni shamba la Mbele,*
*Migogoro tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 57 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. *Jamani tuelimike, sisi sote tuwamoja,*
*Biashara ifanyike, tuungane kwa pamoja,*
*Mshikamano tushike, na kuujenga umoja,*
Migogoro *tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

4. *Mila potofu tuachane, migogoro kuchochea,*
*Kwa umoja tuungane, wizi kuupotezea,*
*Wanakoo tupambane, dhuluma kuondolea,*
*Migogoro tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

5. *Migogoro kutatua, njia majadiliano,*
*Matatizo kuyajua, suluhu bila lumbano,*
*Vikao vyenye kutua, kuitisha bila neno,*
*Migogoro tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

6. *Jambo likishindwa huko, vyombo vya sheria kwenda,*
*Kwa nini tufike huko, migogoro sije kwenda,*
*Kiongozi wa ukoo, migogoro sije panda,*
*Migogoro tuepuke, ukoo kuimarisha. x2*

### Zoezi la 6

1. Ni migogoro gani iliyotajwa katika wimbo huu?
2. Ni migogoro ipi inayojitokeza kwa sasa katika koo zetu ambayo haikutajwa?
3. Umewahi kushuhudia mgogoro wowote wa ndugu katika ukoo? Ni upi?
4. Kuna njia gani nyingine zinazotumika kutatua migogoro katika ukoo wenu?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

(a) Pata majina ya wanaukoo kutoka katika familia yako, kisha chora mti wa ukoo wenu.

(b) Uliza wazazi au walezi wako kuhusu migogoro ya ukoo wenu inavyotatuliwa. Wasimulie wenzako darasani.

## Jamii za kale za ujima

*Soma mazungumzo kati ya Ujima na Masoko, kisha jibu maswali.*

**Masoko:** Habari za leo ndugu?

**Ujima:** Nzuri, sijui wewe?

**Masoko:** Nzuri. Samahani ndugu, naomba kufahamu japo kwa ufupi habari zako.

**Ujima:** Habari zangu! Kuhusu nini?

**Masoko:** Jina lako, tabia au sifa zako na hali ya uhusiano wako.

**Ujima:** Ahaa! Sawa, nitakueleza ila unisikilize kwa makini sana.

**Masoko:** Sawa, hakuna shida.

**Ujima:** Mimi ninaitwa Ujima. Ni mfumo wa kwanza wa kiuchumi na kiutawala ambapo watu waliishi na kushirikiana pamoja. Kila jamii hapa duniani ilipitia katika mfumo huu.

**Masoko:** Ahaa! Safi sana. Jina lako zuri sana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ujima:** Asante sana. Uzuri wangu si wa jina tu, bali ninazo sifa na tabia nyingi.

**Masoko:** Eeeh! Zipi hizo?

**Ujima:** Katika mfumo wangu, umiliki wa mali kama mifugo na ardhi ulikuwa wa pamoja. Hivyo hapakuwa na umiliki binafsi. Hapakuwa na ubaguzi wala matabaka baina yetu. Watu wote walikuwa sawa bila kujali jinsi au rika.

**Masoko:** Mlifanyaje kazi zenu?

**Ujima:** Hapakuwa na mgawanyo wa kazi katika kutengeneza zana, uwindaji na ukusanyaji wa matunda.

**Masoko:** Zana za uzalishaji zilikuwaje?

**Ujima:** Mh! Kwa kweli zana zangu zilikuwa duni sana.

**Masoko:** Kwa nini?

**Ujima:** Kwa sababu zilitengenezwa kwa mawe na miti. Hii ilisababisha kuwepo kwa uzalishaji mdogo.

**Masoko:** Ni mambo gani yalijenga uhusiano katika mfumo wako wa ujima?

**Ujima:** Uhusiano ulikuwa wa kawaida sana. Hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa baina ya watu katika jamii. Hii ilitokana na kukosekana kwa ziada wakati wa kuzalisha.

**Masoko:** Uongozi wako ulikuwaje?

**Ujima:** Uongozi ulikuwa mikononi mwa rika ambapo muundo wa majukumu katika jamii ulifanana.

**Masoko:** Kweli wewe mahiri.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ujima:** Si hivyo tu, enzi zangu hakukuwa na unyonyaji wala ukandamizaji miongoni mwa watu.

**Masoko:** Wewe ulionekana zaidi katika jamii zipi hapa nchini?

**Ujima:** Jamii zote ziliishi na mimi. Hata sasa jamii kama vile Wasandawe, Wahadzabe na Watindiga kutoka jamii za kitanzania bado nipo nao.

**Masoko:** Kwa kweli nimekuelewa vizuri.

**Ujima:** Nakushukuru pia kwa kunielewa.

## Zoezi la 7

1. Kutokana na mazungumzo uliyosoma, nini maana ya ujima?
2. Taja tabia tano zinazopatikana katika jamii zilizopitia mfumo wa ujima.
3. Ni tabia gani umezipenda katika jamii za mfumo wa ujima?
4. Ni matendo gani hukuyafurahia katika jamii za mfumo wa ujima?

### Kazi ya kufanya

Chunguza jamii unamoishi kama kuna mambo yanaonesha tabia za ujima, kama yapo, yaandike na kuyawasilisha kwa wenzako darasani.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 61 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Jamii za kale za ukabaila

Bila shaka umeuelewa mfumo wa maisha wakati wa ujima. Sasa utajifunza mfumo wa ukabaila.

*Fuatilia mazungumzo kati ya babu na mjukuu wake, kisha jibu maswali.*

**Babu:** Mjukuu wangu, leo nina furaha sana. Nataka nikusimulie mambo ya zamani.

**Mjukuu:** Mambo ya zamani! Mambo yapi babu?

**Babu:** Hapo zamani za kale kulikuwa na mfumo wa maisha ulioitwa ukabaila.

**Mjukuu:** Eeeh! Ukabaila ndiyo nini?

**Babu:** Ukabaila ni mfumo wa uchumi na utawala ambao ardhi ilikuwa msingi mkuu wa uzalishaji mali.

**Mjukuu:** Mmh! Huu mfumo ulikuwaje?

**Babu:** Katika mfumo huu, ardhi ilimilikiwa na watu wachache waliojulikana kama makabaila.

**Mjukuu:** Makabaila! Ndio watu gani?

**Babu:** Hawa walikuwa ni watu waliomiliki ardhi na kuwafanyisha kazi watwana.

**Mjukuu:** Eeeh! Watwana tena! Hao nao walikuwa watu gani?

**Babu:** Watwana walikuwa watu wasiokuwa na ardhi; walifanya kazi kwa makabaila. Hivyo walikodi ardhi kwa makabaila na kulipa kodi.

**Mjukuu:** Sasa babu mliishije? Maana naona kama maisha yalikuwa magumu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Babu:** Tuliishi vivyo hivyo kwa kuvumilia.

**Mjukuu:** Kweli zamani kulikuwa na mambo!

**Babu:** Kulikuwa na maisha magumu. Hata watwana waliozalisha mali hawakuimiliki.

**Mjukuu:** Mmh! Kwa namna hii, makabaila na watwana walipendana kweli?

**Babu:** Yaani mjukuu wangu, hawakupendana hata kidogo. Hii ni kwa sababu kulikuwa na unyonyaji baina ya watu. Watwana walinyonywa na kubaguliwa na makabaila.

**Mjukuu:** Mmh! Kwa namna gani?

**Babu:** Watwana walilipa kodi kwa njia ya mazao na kufanyishwa kazi nyumbani kwa makabaila.

**Mjukuu:** Lengo la kuzalisha mali lilikuwa ni nini?

**Babu:** Watu walizalisha kwa ajili ya chakula tu. Ila ziada iliyopatikana ilitumiwa kwa ajili ya biashara.

**Mjukuu:** Jamii gani hasa zilipitia mfumo huo?

**Babu:** Baadhi ya jamii zilizopitia mfumo wa ukabaila zilikuwa ni Wahaya na Waha. Pia, Wapare, Wachaga, Wahangaza na Wanyambo.

**Mjukuu:** Mh! Maisha hayo ya unyonyaji mimi nisingeyaweza.

**Babu:** Hapana, ungeliweza. Mbona mimi niliyaweza na kuishi hadi leo!

**Mjukuu:** Kweli babu umeona mengi ya zamani.

**Babu:** Na bado naendelea kuyaona mengine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

1. Kutokana na mazungumzo uliyosoma, nini maana ya ukabaila?
2. Taja tabia nne za ukabaila zilizobainishwa katika mazungumzo.
3. Ni mambo gani uliyoyapenda katika jamii za ukabaila?
4. Taja mambo mawili ambayo hukuyapenda katika jamii hizi za ukabaila.
5. Shughuli gani za uzalishaji mali zilizofanyika katika mfumo wa ukabaila?

### Kazi ya kufanya

Chunguza jamii unayoishi, kisha bainisha tabia za ukabaila. Ziandike na kuziwasilisha kwa wenzako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Toa maana ya maneno yafuatayo:
   (a) Ukoo
   (b) Uhusiano
   (c) Makabaila
   (d) Watwana
2. Orodhesha matendo matatu yanayoonesha ushirikiano.
3. Taja sifa tatu za mfumo wa ujima.

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

4. Katika maisha yetu ya kila siku hatutakiwi kuwa na uhusiano mwema.__________________
5. Watoto wa kiume wa mzee Kingu ndiyo wanaukoo wa Rushashele.____________________
6. Ukabaila ni mfumo wa kwanza wa kiuchumi katika hatua na mabadiliko ya maendeleo ya kibinadamu._____________
7. Kukaa vikao vya usuluhishi, kuunda kamati za ulinzi, kuwekea mipaka, na kutumia wazee wa kimila ni njia za kutatua migogoro.__________________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Chagua jibu sahihi kutoka* **safu B** *kwa kuandika herufi katika sehemu zilizo wazi* **safu A.**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 8. Wamiliki mali katika ukabaila ni________ | (a) hawabaguani |
| 9. Jamii zilizofuata mfumo wa ukabaila ni_____________ | (b) Wahadzabe, Watindiga na Wasandawe |
| 10. Uhusiano_____________ | (c) watawala |
| 11. Ardhi ndio msingi wa uzalishaji mali___________ | (d) Wahaya, Waha, Wanyambo |
| 12. Mali ilimilikiwa na watu wote______________ | (e) ukabaila |
| 13. Ubaguzi katika maisha______________ | (f) ushirikiano na umoja |
| 14. Kazi za jamii za ujima____ | (g) ujima |
| 15. Wakati wa ujima_________ | (h) ulikuwa kiwango cha chini |
| 16. Mshahara wa mtwana___ | (i) zilifanywa na watu wote |
| | (j) makabaila na watwana |
| | (k) walitumia kila kitu |
| | (l) hapakuwa na ubaguzi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye mabano.**

17. Uhusiano ni_______________
    (a) hali ya watu wawili na zaidi wenye malengo ya pamoja.
    (b) hali ya kugombana baina ya mtu na mtu. ( )
    (c) hali ya kufanya kazi peke yako.

18. Kazi anazosaidia Sekeke nyumbani kwao ni:__________
    (a) Kucheza mpira.
    (b) Kutembea mtaani. ( )
    (c) Kuosha vyombo, kufua na kupika chakula.

19. Kibonge anaporudi kutoka shuleni hufanya nini?_______
    (a) Huuliza kama wamekula.
    (b) Humbeba mdogo wake na kucheza naye. ( )
    (c) Hugombana na wenzake.

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Kodi: | malipo yanayotozwa baada ya kupanga na kutumia kitu kwa muda |
| Kufariji: | kuliwaza mtu wakati wa tabu au huzuni |
| Matabaka: | mgawanyo wa watu kimakundi kufuatana na hali yao ya elimu au utajiri |
| Mfumo: | utaratibu wa utendaji au utekelezaji wa jambo fulani |
| Sabika: | jambo ambalo kamwe halikuwahi kushuhudiwa |
| Suluhisho: | uamuzi unaofanywa na kuleta upatanisho baina ya pande mbili zilizogombana |
| Ukabaila: | mfumo wa maisha ambao watu wachache humiliki ardhi |
| Unyonyaji: | hali au tabia ya mtu kupata mapato bila ya kufanyia kazi |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 67 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Mashujaa wetu

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza habari za viongozi wakuu wa serikali ya Tanzania waliowahi kuongoza tangu wakati wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hapo mwaka 1964. Ulichambua pia mchango wao kwa taifa la Tanzania. Katika sura hii, utajifunza tabia za kishujaa na namna ya kuwatambua mashujaa wetu. Pia, utawafahamu mashujaa wa zamani waliopinga uvamizi wa taifa letu. Vilevile, utajifunza sababu zilizowafanya mashujaa hao kupinga uvamizi wa taifa letu. Mwisho, utajifunza mchango wao na namna ya kuwaenzi katika taifa la Tanzania.

### Tabia za kishujaa

Kila jamii inaweza kuwa na mtu shujaa. Hata wewe siku moja unaweza kuwa shujaa. Shujaa anaweza kuwa kijana au mzee, mwanaume au mwanamke.

**Soma hadithi, kisha jibu maswali.**

Jonas, Merina na Abdul ni vijana marafiki wa muda mrefu. Vijana hao walizaliwa katika Kijiji cha Makele. Walikuwa na tabia nzuri, moyo wa upendo, uzalendo na ujasiri katika kijiji hicho.

Siku moja kijiji chao kilivamiwa na wezi usiku wa manane. Wezi hao waliiba mifugo ya wanakijiji ikiwa ni pamoja na ng'ombe,

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 68 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kondoo na mbuzi. Wanakijiji walilalamika sana siku hiyo. Siku iliyofuata, vijana hao waliamua kuwafuatilia wezi wa mifugo. Walitembea na kukimbia umbali mrefu bila kuchoka. Walikuwa wamebeba silaha za jadi kama vile mapanga, mikuki na visu. Wakiwa njiani walikumbana na wanyama wakali kama simba na chui. Lakini vijana hawa walipambana na wanyama na kuwashinda.

Baada ya mwendo wa siku mbili wakiwa wamechoka, waliona kundi la mifugo kwa mbali. Walipokuwa wanaikaribia mifugo ghafla walivamiwa na kundi la wezi walioiba mifugo hiyo. Wezi walianza kuwashambulia Jonas na rafiki zake. Vijana walipambana na wezi kwa kutumia mikuki na mapanga kwa muda wa saa moja. Kwa ujasiri wao vijana walifanikiwa kuwapiga wezi hao na kuwakimbiza. Hatimaye vijana waliikomboa mifugo hiyo na kuanza safari ya kurudi kijijini kwao.

Walipofika kijijini kwao walishangiliwa kwa nderemo na vifijo. Wanakijiji waliwaimbia nyimbo nzuri za kuwasifu vijana kwa kuwa jasiri na imara. Watu walisikika wakiimba “Nyie ni vijana shupavu, wavumilivu na wakombozi wa jamii”. Waliwasifu vijana hao kwa kujitoa muhanga kwa ajili ya watu wa kijiji chao. Ama kweli, Jonas na wenzake walikuwa mashujaa.

Shujaa hutumia akili yake, kipaji chake na nguvu zake ili kusaidia jamii nyakati za matatizo. Hivi vyote huchangia kuleta maendeleo ya jamii yake. Wakati mwingine hujitoa muhanga katika kulinda rasilimali, heshima na ustawi wa jamii yake. Shujaa hufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba jamii yake inabaki salama wakati wote.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 69 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shujaa huwa na tabia ya upendo na moyo wa kizalendo. Hutetea na kulinda jamii yake, wala hakati tamaa kwa jambo lolote. Hivyo, shujaa huwa mstari wa mbele kupambana kwa faida ya jamii.

## Zoezi la 1

1. Kutokana na hadithi hiyo uliyoisoma, nini maana ya mtu shujaa?
2. Taja tabia nne za kishujaa zilizoelezwa katika hadithi uliyoisoma.
3. Ni matendo gani zaidi ya kishujaa unayoyafahamu?
4. Je, shuleni kwako kuna wanafunzi wenye tabia kama za vijana uliowasoma? Wataje na vitendo vyao vya ushujaa.
5. Ni matendo gani unayoweza kuyafanya shuleni kwako yakakupa sifa ya kuitwa shujaa?
6. Taja tabia tano za kishujaa unazoweza kuzitenda katika familia yako.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya kufanya

Uliza wazazi au walezi juu ya mtu aliyewahi kufanya matendo ya kishujaa. Shirikiana na wanafunzi wenzako kuigiza matendo hayo darasani.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 70 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mashujaa wa kale waliopinga uvamizi wa taifa letu**

Hapo mwanzo tumesoma kwamba shujaa hulinda na kutetea watu wake. Pia, huwa mstari wa mbele kupinga uonevu wa aina yoyote. Hivyo, mashujaa wetu wengi waliwahi kupinga uonevu na uvamizi wa taifa letu.

**Soma habari hii, kisha jibu maswali.**

Mwaka 1886 hadi mwaka 1918, wajerumani walivamia na kutawala eneo lililojulikana kama Tanganyika. Eneo hilo, waliliita Koloni la Wajerumani ya Afrika Mashariki.

Wajerumani waliivamia Tanganyika ili kutafuta ardhi ya kulima mazao ya biashara. Pia, walihitaji malighafi kama vile mpira, kahawa na dhahabu kwa ajili ya viwanda vyao huko Ulaya. Aidha, walihitaji masoko ya kuuzia bidhaa za viwanda vyao. Vilevile, walihitaji wafanyakazi wa mashambani na migodini.

Uvamizi huo uliibua migogoro mikubwa kati ya wavamizi na wenyeji. Wajerumani walichukua ardhi ya wananchi kwa nguvu na kuwafanyisha kazi kwa muda mrefu. Baadhi ya wananchi walilipwa ujira kidogo na wengine hawakulipwa kabisa. Wengine walichapwa viboko na wengine kunyongwa. Pia, wananchi walitozwa kodi na kulazimishwa kulima baadhi ya mazao ya biashara. Kwa vile uvamizi huo uliwaumiza wananchi katika nchi yao, hivyo waliamua kuupinga. Hali hii ilijenga chuki na uadui mkubwa kati ya wajerumani, wananchi na viongozi wao.

Wananchi waliamua kupambana na kuupinga uvamizi wa wajerumani bila kuogopa. Walishirikiana na mashujaa wao kupambana bila kukata tamaa. Mashujaa wengi wa Tanganyika

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 71 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

walisimama mstari wa mbele kukataa utawala wa wavamizi. Ushujaa wao ulibainika kutokana na matendo waliyoyafanya kwa jamii zao.

## Mashujaa wa Tanganyika

Angalia jedwali uwatambue mashujaa wetu na maeneo waliyopinga uvamizi.

| Na | Jina la Shujaa | Mahali |
|---|---|---|
| 1. | Hassan Bin Omari Makunganya | Kilwa - Kivinje |
| 2. | Bwana Heri | Uzigua - Tanga |
| 3. | Abushiri Bin Sultani | Pangani - Tanga |
| 4. | Mangi Meli | Moshi - Kilimanjaro |
| 5. | Mkwawa | Iringa |
| 6. | Kinjekitile Ngwale | Umatumbi- Kilwa |
| 7. | Isike | Unyanyembe -Tabora |
| 8. | Mangi Sina | Kibosho - Kilimanjaro |
| 9. | Mirambo | Tabora |
| 10. | Machemba | Uyao - Mtwara/Lindi |

Mashujaa waliotajwa katika jedwali walionesha ujasiri na ukakamavu katika kupinga utawala wa wajerumani. Mashujaa hawa walikuwa na moyo wa kizalendo. Hawakupenda kuona watu wao wakitawaliwa na kunyanyaswa na wavamizi. Walijitoa muhanga kupambana na wavamizi hao. Mashujaa hawa walitumia akili, vipaji na nguvu zao kupambana na wageni. Walipambana na wavamizi kufa au kupona.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 72 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, waliwahamasisha watu kupambana dhidi ya wavamizi hao. Walitumia silaha za jadi kama vile mikuki, pinde, mishale na mapanga kuwapiga wavamizi. Baadhi yao walitumia gobore na mawe. Mashujaa hao waliunda vikosi vya askari ili kupambana na wavamizi. Wajerumani wakatambua kwamba nchi hii ilikuwa na wenyewe. Kwa hiyo ili kushinda mapambano, walitakiwa kujipanga upya mara kwa mara.

## Zoezi la 2

1. Ni jambo gani kubwa lililowafanya mashujaa wa Tanganyika waupinge uvamizi wa kijerumani?
2. Taja tabia nne za kishujaa walizoonesha mashujaa wetu kipindi cha uvamizi wa kijerumani.
3. Ni tabia gani za kishujaa ulizonazo wewe?
4. Orodhesha sababu nne zilizowafanya wajerumani kuja Tanganyika.
5. Tabia gani ya kishujaa unaweza kuijenga kutokana na mashujaa uliowasoma?

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako mbinu mtakazozitumia kujikinga na maadui. Andika kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Changamoto katika kupinga utawala wa wajerumani

Katika mapambano ya kupinga kitu fulani, changamoto hujitokeza. Katika kupinga uvamizi wa wajerumani, mashujaa na wananchi walikumbana na changamoto nyingi. Wakati wa kupinga uvamizi wa kijerumani Tanganyika, mbinu mbalimbali zilitumika. Jamii nyingi za Tanganyika zilitumia mbinu za kivita kupinga uvamizi. Katika mbinu hii, wananchi walitumia silaha za jadi. Wakati huohuo, wajerumani walitumia mizinga na bunduki kuwapiga wananchi wa Tanganyika.

Wakati wa kupinga uvamizi wa wajerumani, wananchi walikumbwa na changamoto nyingi. Changamoto hizo ni pamoja na kuwa na silaha duni na ukosefu wa mbinu sahihi za kivita. Pia, uwepo wa imani potofu za kivita baina yao na kukosa umoja. Juhudi za kujikomboa tangu wakati huo, iliwezesha pia wananchi hawa kudai uhuru. Tanganyika ikapata uhuru mwaka 1961. Taifa letu linajivunia uongozi bora wa mashujaa wetu.

Hata jamii za sasa zinakabiliwa na changamoto kadhaa za kupambana na uvamizi. Moja ya changamoto ni ukosefu wa mwamko wa watu katika kutatua migogoro kwa njia ya amani bila vita. Pia, jamii hizi zina changamoto za watu wengi kutokujua sheria za kufuata na kudai haki. Vilevile, watu wengi wa sasa wanakosa uzalendo.

Ni vema kutambua kuwa kupinga uvamizi ni jambo muhimu. Lakini vita siyo mbinu nzuri ya kupigania haki. Migogoro inaweza kutatuliwa kwa njia ya amani kama vile mazungumzo

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 74 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na mahakama. Umoja na ushirikiano ni nguzo muhimu katika kutatua migogoro kwenye jamii.

## Zoezi la 3

1. Bainisha njia iliyotumika kupinga uvamizi wa wajerumani.
2. Taja changamoto tatu zilizosababisha jamii za Tanganyika kushindwa vita dhidi ya wajerumani.
3. Taja silaha walizotumia mashujaa wetu katika kupigana na wajerumani.
4. Ni njia zipi nyingine unazozifahamu zinazoweza kutumika katika kutatua migogoro?
5. Orodhesha hatua za kufuata unapoonewa shuleni.

### Kazi ya kufanya

(a) Jadiliana na mwenzako darasani nini kingetokea kama mashujaa wetu wangekuwa na umoja?

(b) Uliza wazazi au walezi kuhusu historia ya uvamizi katika jamii yako. Andika kwenye daftari lako kisha waeleze wenzako darasani.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 75 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Uvamizi baina ya jamii katika taifa letu**

Sura zilizopita zilionesha migogoro mbalimbali katika jamii. Ni vema ukatambua kuwa chanzo kimojawapo cha migogoro hiyo ni uvamizi.

**Soma habari hii, kisha jibu maswali.**

Watu katika jamii nyingi za Tanzania hupenda kuvamia maeneo yenye kuwaletea faida. Hivyo, uvamizi wa maeneo baina ya jamii na jamii huleta migogoro. Migogoro hiyo huweza kuleta mapigano yenye kuhusisha silaha. Hata leo, ipo migogoro ya kivamizi inayojitokeza katika jamii zetu. Ipo migogoro baina ya mtu na mtu au familia na familia. Wakati mwingine baina ya kabila moja na jingine.

Watu wa jamii ya wakulima wamekuwa na migogoro na jamii za wafugaji. Migogoro katika jamii hizi hutokana na kugombania ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Katika jamii zetu ipo pia migogoro kati ya wananchi wa eneo fulani na wawekezaji au serikali. Migogoro hii hutokana na uvamizi wa wawekezaji kwenye ardhi halali ya wananchi. Upo uvamizi unaohusisha wawekezaji kuchukua ardhi bila kibali cha serikali. Wakati mwingine wananchi huvamia maeneo ya wawekezaji au ya serikali bila ruhusa. Mara zote maeneo muhimu ndiyo huvamiwa.

Watu hupenda kuvamia maeneo yenye madini na ardhi nzuri kwa kilimo na ufugaji. Pia, hupenda sehemu zenye hifadhi za wanyama na sehemu zilizo karibu na barabara. Vilevile, hutafuta maeneo kwa ajili ya kilimo, ufugaji, ujenzi wa nyumba

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 76 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

za kuishi au uchimbaji madini. Watu wengine hutafuta maeneo ya kufanyia biashara na vyanzo vya maji. Hali hii husababisha kutokea migogoro katika jamii husika. Migogoro inapotokea, inahitaji watu wenye tabia za kishujaa ili kuweza kuitatua.

Migogoro inapotokea katika jamii zetu ni muhimu kusuluhishwa kwa haraka. Pia, zitumike mbinu nzuri zinazoleta utulivu katika jamii. Mbinu kama vile kutunga sheria na kuweka vikao vya baraza hutumika. Jamii zingine huweka mipaka katika ardhi, huunda kamati za ulinzi na usalama. Mbinu hizi zote hupunguza migogoro katika jamii husika. Ni vema kutatua migogoro ili kuleta amani, furaha na upendo ndani ya jamii.

## Zoezi la 4

1. Katika habari uliyoisoma, umebaini ni migogoro gani ya uvamizi ipo katika jamii zetu?
2. Taja migogoro miwili ya uvamizi iliyopo katika jamii ambayo haikutajwa kwenye habari uliyoisoma.
3. Je, wewe unaweza kutatua mgogoro au tatizo gani katika jamii yako?
4. Je, ukitokea mgogoro wa mipaka kati ya shule yako na mwananchi jirani, utafanya nini?

### Kazi ya kufanya

(a) Uliza kwa walezi au wazazi katika jamii unayoishi kuhusu:
  (i) Uvamizi au migogoro iliyopo sasa.
  (ii) Chanzo cha migogoro hiyo na jamii zinazohusika.
  (iii) Mbinu zinazotumika kutatua migogoro hiyo.
  Simulia wenzako darasani.

(b) Jadiliana na wenzako kuhusu njia zitakazosaidia kutatua migogoro endapo itajitokeza shuleni kwenu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 77 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mchango wa mashujaa wetu

Imba wimbo unaofuata kubaini mchango wa mashujaa wetu.

1. *Leo siku imefika, uwanjani kuwambia,*
   *Mashujaa wakumbukwa, mchango wao sikia,*
   *Ujasiri lotukuka, mshikamano achia,*
   *Twawapenda mashujaa, mchango wenu twa tambua. x 2*

2. *Mambo mengi mmefanya, taifa kutuletea,*
   *Haki zetu mekusanya, uhuru kutujengea,*
   *Uzalendo kukusanya, uonevu ondolea,*
   *Twawapenda mashujaa, mchango wenu twa tambua. x 2*

3. *Hofu kwetu kuondoa, usalama kuujenga,*
   *Mali zetu kukomboa, matatizo kutojenga,*
   *Ni amani kuongoa, unyonyaji kuupinga,*
   *Twawapenda mashujaa, mchango wenu twa tambua. x 2*

### Zoezi la 5

1. Ni mchango gani uliotolewa na mashujaa wetu uliotajwa kwenye wimbo?
2. Wimbo uliosoma unakufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 78 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kuwaenzi mashujaa wetu**

Mashujaa wetu walikuwa na mchango mkubwa katika jamii zetu. Hivyo yatupasa kuwaenzi kwa njia mbalimbali.

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.**

Katika nchi yetu ya Tanzania, mashujaa wetu huwa tunawaenzi kwa kuimba nyimbo za kuwasifu. Pia, tunasherehekea Sikukuu ya Mashujaa kitaifa. Sikukuu hii hufanyika kila mwaka tarehe 25 mwezi wa saba. Vilevile, tunawasifu kwa kuandika habari zao na kuzitunza.

Wakati mwingine huwaenzi kwa kuiga matendo mema waliyoyafanya. Vivyo hivyo, tunawaenzi kwa kuandika majina yao katika maeneo mbalimbali katika jamii. Maeneo hayo yanaweza kuwa majina ya barabara, shule, vikosi vya jeshi, mabweni na mitaa. Kwa kufanya hivyo, tunaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi kwa matendo waliyoyafanya.

**Zoezi la 6**

1. Taja njia tano tunazozitumia kuwaenzi mashujaa wetu.
2. Tunga wimbo wa kuwasifia mashujaa wetu na uwaimbie wenzako darasani.
3. Orodhesha majina ya barabara, shule, kijiji/mtaa au hospitali zilizo na majina ya mashujaa.

**Kazi ya kufanya**

Shirikiana na wenzako darasani kufanya yafuatayo:

(a) Tunga na kuimba wimbo wa kusifia mashujaa wetu.

(b) Igiza matendo au tabia za kishujaa.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 79 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Ni mambo gani yanayosababisha jamii moja kuivamia jamii nyingine?
2. Orodhesha migogoro inayojitokeza katika jamii yako ambayo haikutajwa katika sura hii.
3. Eleza tabia unazoweza kujenga kutokana na ujumbe ulioupata katika sura hii.
4. Kama ungekuwepo wakati wajerumani wanaivamia Tanganyika, ungefanya nini?
5. Taja tabia tano za kishujaa unazoweza kuzitenda katika jamii yako.

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

6. Mashujaa wetu hukumbukwa kwa kusherehekea sikukuu ya mashujaa.______
7. Mzalendo yeyote anatakiwa kuwa shujaa wa taifa lake.__
8. Mojawapo ya sababu zilizofanya jamii zetu kushindwa katika vita dhidi ya wajerumani ni silaha duni._______
9. Njia nzuri ya kutatua migogoro ni vita.___________
10. Kinjekitile alikuwa ni shujaa wa watu wa Iringa._________
11. Shujaa hutoa maisha yake yote kwa ajili ya watu wengine.________
12. Shujaa hukimbia matatizo pale yanapotokea._______
13. Mashujaa wengi katika jamii hutuletea matatizo.______
14. Shujaa huwaongoza watu wake kupambana bila kukata tamaa.________
15. Shujaa lazima awe na nguvu za kupigana kuliko watu wote.________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika mabano.**

16. Tanganyika ilitawaliwa na wajerumani tangu mwaka _______
    (a) 1886 hadi 1961.
    (b) 1885 hadi 1907.
    (c) 1919 hadi 1945.
    (d) 1886 hadi 1918. ( )

17. Ni njia gani unaweza kuzitumia ili kupata taarifa za mashujaa katika jamii?_________________
    (a) Kwa kusoma na kuhadithiwa habari zao.
    (b) Kwa kuangalia nyuso zao.
    (c) Kwa kuangalia miili yao kama ina nguvu.
    (d) Kwa kuota ndoto. ( )

18. Kinjekitile Ngwale aliongoza mapambano ya kupinga uvamizi wa wajerumani katika mikoa ipi?___________
    (a) Mwanza na Shinyanga.
    (b) Tabora na Pwani.
    (c) Mtwara na Lindi.
    (d) Pwani na Tanga. ( )

19. Moja ya sababu zilizowafanya wajerumani kuvamia Tanganyika ilikuwa_________________
    (a) kueneza Dini ya Kiislamu.
    (b) upendo wa wajerumani kwa watanzania.
    (c) kutafuta masoko ya bidhaa zao.
    (d) kuimarisha misingi ya uzalendo. ( )

20. Mtemi Isike aliongoza kabila gani kuwapinga wajerumani?
    (a) Wasukuma.
    (b) Wanyamwezi.
    (c) Wazaramo.
    (d) Wahehe. ( )

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 81 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Andika herufi ya jibu sahihi kutoka* **kifungu B** *kwa kuoanisha na* **kifungu A.**

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| 21. _______ kunasaidia kuepuka migogoro katika jamii. | (a) maeneo yenye madini, ardhi kubwa na kwenye vyanzo vya maji |
| 22. ______ ni chanzo kikubwa cha migogoro. | (b) Uvamizi |
| 23. Uvamizi hufanyika _______. | (c) Wafugaji na wakulima |
| 24. Jamii zenye migogoro mingi hapa nchini _______. | (d) Kuheshimu mipaka |
| | (e) Kutafuta masoko |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Duni: | dhaifu |
| Gobore: | bunduki ya kizamani yenye mtutu mrefu wa kushindilia na kufyatua risasi |
| Jadi: | kitu chochote cha asili ya mtu kwa mujibu wa mazingira anakotoka |
| Malighafi: | mali ambayo hutumika kutengenezea vitu vingine |
| Muhanga: | mtu anayehatarisha maisha yake kwa ajili ya kupigania maslahi yake, ya mtu, jamii au nchi yake au nchi nyingine |
| Nderemo: | hali ya kuwa na furaha inayoendana na kelele za shangwe |
| Potofu: | kwenda tofauti na utaratibu |
| Shujaa: | mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabiliana na mambo bila woga |
| Ujasiri: | hali ya kukabili jambo bila hofu, tena kwa uhodari |
| Uvamizi: | kuingia na kumiliki sehemu isiyo yako kwa kutumia nguvu |
| Uzalendo: | hali ya mtu kuwa tayari kutumikia na kuitetea nchi yake |
| Vifijo: | kelele za shangwe na vigelegele |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kutumia ramani katika mazingira

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza kuchora picha za vitu halisi vilivyomo darasani. Pia, ulijifunza kuchora ramani za vitu mbalimbali vinavyopatikana katika maeneo ya shule. Katika sura hii, utajifunza alama za ramani na jinsi ya kuchora ramani ya shule. Vilevile, utajifunza kuchora pande kuu nne za Dunia. Mwisho, utajifunza kusoma uelekeo wa vitu katika mazingira kwa kutumia pande kuu nne za Dunia.

### Alama za ramani

Unapotaka kuchora vitu halisi katika ramani, unapaswa kutumia alama za vitu hivyo. Tunatumia alama za ramani kuwakilisha vitu halisi. Tunafanya hivyo kwa sababu ya ukubwa wa kitu halisi chenyewe kikilinganishwa na ukubwa wa karatasi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 84 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Chunguza ramani ifuatayo ili uweze kutambua alama za ramani.*




**Kielelezo namba 1:** *Ramani ya Shule ya Msingi Kidare*

## Zoezi la 1

1. Taja vitu vilivyomo katika ramani ya Shule ya Msingi Kidare.
2. Chora alama za vitu vifuatavyo kama vinavyoonekana katika ramani iliyochorwa;
   (a) mto,
   (b) daraja,
   (c) barabara kuu,
   (d) bustani ya matunda,
   (e) nyumba za kuishi.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 85 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kutokana na ramani hii umeona kwamba, vitu halisi huweza kuwakilishwa kwa michoro. Kwa hivyo, michoro inayowakilisha vitu halisi katika ramani huitwa alama za ramani. Alama zinazotumika katika ramani ni muhimu na maalumu. Alama hizi huwakilisha vitu vinavyopatikana katika mazingira halisi ya eneo husika. Alama huwakilisha kitu fulani kama vile kanisa, msikiti**,** tangi la maji, mto na mlima. Pia, huwakilisha nyumba daraja, reli, na njia ya miguu. Vilevile, huwakilisha mpaka wa kijiji, bustani ya miti, mashamba ya kijiji na kisima cha maji.

## Ramani ya shule yetu

Ramani ni muhimu katika mazingira. Uchoraji wa ramani ni stadi muhimu katika kuelewa maeneo, mipaka, rasilimali, mito na barabara. Unaweza kuchora ramani ya kitu halisi kwa kutumia picha ya kitu hicho. Pia, unakumbushwa kuwa ramani ya kitu halisi huchorwa kwa kutumia alama.

**Kazi ya kufanya**

Chora ramani ya Shule ya Msingi Kidare kwenye daftari lako kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1.

Unapochora ramani ya kitu chochote, hakikisha kwamba una vifaa. Vifaa hivyo ni pamoja na penseli, daftari, kifutio na rula. Wakati mwingine unaweza ukawa na picha ya kitu au kitu halisi unachotaka kuchora. Hivyo angalia kwa makini picha hizo na uchore kwa kufuata utaratibu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari ifuatayo ili kujua jinsi ya kuchora ramani.**

Jina langu ni Kachoma. Nasoma Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Mianzini. Mwalimu Mponda hutufundisha somo la Maarifa ya Jamii. Katika darasa letu tupo wanafunzi 40. Miongoni mwa wanafunzi wa darasa letu ni Juma, Tito, Kibure na Mwanaisha.

Siku moja, mwalimu Mponda alitupatia kazi ya kuchora ramani ya shule yetu. Kila mmoja alianza kuchora ramani hiyo katika daftari lake. Siku iliyofuata tulikusanya daftari ili mwalimu azisahihishe. Baada ya kurudishiwa madaftari yetu, mwalimu alimsifia Tito kwa kuwa alichora ramani nzuri.

**Fuatilia mazungumzo yao darasani, kisha jibu maswali.**

**Mwalimu Mponda:** Tito, ulijifunza wapi kuchora ramani?

**Tito:** Kaka yangu anayesoma sekondari ndiye aliyenifundisha kuchora. Ninapenda sana kuchora.

**Mwalimu Mponda:** Aah! Vizuri Tito, njoo mbele ya darasa utuelekeze namna ya kuchora ramani. (*Tito, alikwenda mbele ya darasa na kuwaelekeza wenzake.*)

**Tito:** Unapochora ramani ni lazima uzingatie vipengele vifuatavyo:

**Kwanza, fremu ya ramani au mipaka:** Hii huchorwa kwa kuzungushia eneo la ramani katika mstatili au mraba. Kazi yake ni kuonesha mwisho wa eneo la usomaji wa ramani.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 87 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Pili, ufunguo:** Huandikwa chini ya ramani ili kuonesha orodha ya alama za ramani na maana yake. Ufunguo hutuwezesha kuelewa maana ya vitu vilivyomo katika ramani. Kwa mfano, alama za majengo ya shule, nyumba za walimu na viwanja vya mpira.

**Tatu, kichwa cha ramani:** Hiki huandikwa chini ya ramani ili kutambua jina la eneo lililochorwa. Pia, huonesha madhumuni ya ramani hiyo. Kwa mfano, ramani ya Shule ya Msingi Kidare.

**Nne, dira:** Hii huchorwa katika ramani ili kuonesha uelekeo wa maeneo au vitu mbalimbali katika ramani.

**Na mwisho ni kipimio cha ramani:** Huonesha uwiano kati ya umbali halisi na umbali ulioko kwenye ramani.

**Mwalimu Mponda:** Ohoo! Safi sana Tito. Mwanaisha umeelewa namna Tito alivyofafanua vipengele vya uchoraji wa ramani?

**Mwanaisha:** Ndiyo mwalimu, sasa nimeelewa vipengele vya kuzingatia wakati wa kuchora ramani.

**Mwalimu Mponda:** Nimefurahi kwa maelezo yako Tito. Sasa ngoja niwaelekeze hatua za uchoraji wa ramani. Kila mmoja achukue daftari,

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 88 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kalamu, rula na kifutio. Tuchore ramani yetu kwa vitendo kwa kufuata hatua zifuatazo:

***Hatua ya kwanza:***

Tunatakiwa tuandae na kutumia kipimio cha ramani.

**Kibure:** Mwalimu tunawezaje kutumia kipimio cha ramani?

**Mwalimu Mponda:** Kipimio cha ramani ni uwiano wa umbali kati ya ramani na umbali halisi katika ardhi. Kwa mfano, sentimita moja kwenye ramani inaweza kuwakilisha kilomita mbili kwenye ardhi. Hii ina maana, badala ya kuchora kilomita mbili kwenye karatasi, utachora sentimita moja.

***Hatua ya Pili:***

Tuchore fremu ya ramani katika daftari.

***Hatua yaTatu:***

Tuchore alama za vitu vinavyopatikana katika mazingira ya shule yetu katika fremu. Tumia alama za ramani zinazowakilisha vitu hivyo. Vitu hivyo ni kama bustani za maua, miti ya shule na mlingoti wa bendera. Vitu vingine ni uwanja wa michezo, kisima cha maji, bendera ya shule na majengo.

***Hatua ya Nne:***

Tuchore ufunguo unaoonesha maana ya alama za vitu tulivyochora katika ramani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Hatua ya Tano:***

Tuchore dira upande wa kulia wa ramani.

***Hatua ya Sita:***

Tuandike kichwa cha ramani. Sasa tumechora ramani ya shule yetu.

**Wanafunzi:** Ahaa! asante mwalimu. Sasa tumeelewa.

## Zoezi la 2

1. Ni vipengele vingapi vya kuzingatia unapochora ramani? Vitaje.
2. Eleza hatua za kufuata unapochora ramani.

## Kazi ya kufanya

Chora ramani ya nyumba yenu kwa kuzingatia vipengele vya ramani. Muoneshe ramani hiyo mwalimu wako wa somo la Maarifa ya Jamii.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 90 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Pande kuu nne za Dunia

Kila unapotembea huwa unaelekea upande fulani wa Dunia. Kila upande wa Dunia huwa na jina lake. Dira ya Dunia hutusaidia kutambua uelekeo wa mahali tunapokwenda. Pia, hutusaidia kutambua mahali vitu vilipo kama vile kanisa, msikiti au daraja katika ramani.

**Fanya kazi ifuatayo kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa, ili uweze kutambua kila upande wa Dunia.**

1. Nenda nje ya darasa wakati wa asubuhi.
2. Tazama Jua linakotokea.
3. Weka alama na uchore duara mahali uliposimama mchangani.
4. Tembea hatua tatu mbele ukitazama Jua linapotokea andika neno **Mashariki** kwenye mchanga.
5. Rudi kwenye duara na utembee kwenda nyuma hatua tatu na uandike neno **Magharibi** kwenye mchanga.
6. Rudi tena kwenye duara, simama na uangalie Jua.
7. Geuka mkono wa kulia, tembea hatua tatu andika neno **Kusini.**
8. Rudi tena kwenye duara na uangalie Jua linapotokea. Kisha geuka kushoto kwako utembee hatua tatu mbele na uandike neno **Kaskazini.**
9. Chukua kijiti na uchore mistari iliyonyooka kutoka kwenye kila alama uliyoweka ardhini kuelekea kwenye mduara.
10. Baada ya hapo chunguza huo mchoro kisha chora kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 91 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ulipochora mchoro wako bila shaka mchoro huo ulifanana na alama ya kujumlisha. Hizo ndizo pande kuu nne za Dunia. Pande hizo ni Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi.




**Kielelezo namba 2:** *Pande kuu nne za Dunia*

## Zoezi la 3

1. Kuna faida gani za kutumia pande kuu za Dunia?
2. Jua huonekana kuchomoza kutoka upande gani wa Dunia?
3. Toka ndani ya darasa na utaje upande vilipo vitu vifuatavyo:
   (a) Nyumbani kwenu,
   (b) Ofisi ya mwalimu mkuu,
   (c) Kengele ya shule,
   (d) Vyoo vya wanafunzi wa kiume,
   (e) Kibao cha shule.
4. Eleza nini kingetokea kama kusingekuwepo na pande kuu za Dunia.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 92 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Kwa kushirikiana na mwanafunzi mwenzako, tengeneza kifani cha pande kuu nne za Dunia. Omba maelekezo kutoka kwa wazazi au kwa mwalimu wako wa somo la Maarifa ya Jamii ili utengeneze kifani hicho.

## Kusoma uelekeo wa vitu katika mazingira kwa kutumia pande kuu nne za Dunia

Unapotaka kusoma uelekeo wa vitu katika mazingira, unapaswa kutumia pande kuu nne za Dunia. Pande hizo huoneshwa na alama. Alama hiyo huitwa dira na huonesha Kaskazini ya ramani. Kwa kutumia dira hii ni rahisi kujua upande wa Kusini, Mashariki na Magharibi.

*Chunguza ramani ifuatayo, kisha jibu maswali.*




**Kielelezo namba 3:** *Ramani ya shule*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Ni vitu gani vinapatikana Kaskazini mwa barabara kuu?
2. Shule iko upande gani wa uwanja wa mpira wa miguu?
3. Taja vitu vinavyopatikana Magharibi mwa darasa la kwanza.
4. Jengo la choo liko upande upi wa darasa la IV?

### Kazi ya kufanya

Nenda nje ya darasa lako na uangalie upande iliko nyumba yenu. Angalia pia upande ziliko ofisi za walimu, vyoo vya shule na uwanja wa mpira wa miguu.

## Zoezi la jumla

*Oanisha sentensi kutoka* **safu B** *na maneno sahihi kutoka* **safu A** *ili yalete maana sahihi.*

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 1. Dira __________ | (a) mipaka ya mraba au mstatili |
| 2. Mpaka______ | (b) chombo kitumikacho kuonesha uelekeo wa mahali |
| 3. Ufunguo_____ | (c) michoro au alama zinazotambulisha kitu katika ramani |
| 4. Fremu ________ | (d) orodha ya alama za ramani na maana zake |
| 5. Alama za ramani _______ | (e) mahali ambapo ni kikomo cha eneo au kitu dhidi ya kingine |
| | (f) pande kuu nne za Dunia |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi au* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

6. Kalamu, daftari, kifutio na rula ni vifaa vya kuchorea.______
7. Jua huonekana kuzama upande wa Magharibi.________
8. Katika ramani, dira huoneshwa upande wa kulia mwa ramani._______________
9. Duara ni alama ya msikiti katika ramani.______________
10. Unapochora ramani, ni lazima kuzingatia vipengele vya ramani.________________

**Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuchora picha ya kitu halisi na alama yake.**

| Jina la kitu halisi | Picha ya kitu | Alama ya kitu |
|---|---|---|
| 11. Reli | | |
| 12. Miti | | |
| 13. Kisima | | |
| 14. Mto | | |

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Alama za ramani: | michoro au alama zinazotambulisha kitu katika ramani |
| Mchoro: | umbo lililosanifiwa na kalamu au rangi |
| Mpaka: | mahali ambapo ni kikomo cha eneo au kitu dhidi ya kingine |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Mfumo wa Jua

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza vitu vinavyounda Mfumo wa Jua. Katika sura hii, utajifunza Mfumo wa Jua na kubaini mwanga wa asili katika mazingira. Pia, utajifunza tofauti kati ya mwanga wa Jua na mwanga wa Mwezi.

### Dhana ya Mfumo wa Jua

Mfumo wa Jua ni mkusanyiko wa sayari nane zinazolizunguka Jua. Jua nalo ni sehemu ya mfumo huo. Vitu kama vile nyota, Mwezi, vimondo na sayari huunda Mfumo wa Jua. Sayari hizo ni Zebaki, Zuhura, Dunia, Mirihi, Sumbula, Sarateni, Zohali na Kausi. Jua huwa katikati ya Mfumo wa Jua. Kila sayari hulizunguka Jua katika njia yake iitwayo Obiti. Vitu vingine katika Mfumo wa Jua ni kama Asteroidi, Meteoridi na Kometi.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 96 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha ifuatayo, kisha imba shairi.*




**Kielelezo namba 1:** *Mfumo wa Jua*

Imba shairi lifuatalo, ili uweze kuelewa mpangilio wa sayari katika Mfumo wa Jua.

1. *Sisi sayari twatua, uwanjani tumetua,*
   *Habari nzuri twajua, mfumo Jua kujua,*
   *Sayari zote jijua, tuko wanane tambua,*
   *Ya kwanza hadi ya nane, sote twazunguka Jua.*

2. *Kwa pamoja tumetaja, mpangilio wa hakika,*
   *Ninaanza namba moja,* **Zebaki** *wa kusifika,*
   *Namba mbili ninakuja,* **Zuhura** *ninazunguka,*
   *Ya kwanza hadi ya nane, sote twazunguka Jua.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. **Dunia** *nawaambia, namba tatu nazunguka,*
*Wa nne nafuatia,* **Mirihi** *natambulika,*
**Sumbula** *nimeingia, mkubwa sana sikika,*
*Ya kwanza hadi ya nane, sote twazunguka Jua.*

4. *Mwenye pete natokea,* **Sarateni** *mwaniona,*
**Zohali** *natokezea, ninang'ara kuwaona,*
**Kausi** *ninatokea, ni wa mwisho kuniona,*
*Ya kwanza hadi ya nane, sote twazunguka Jua.*

## Zoezi la 1

1. Katika Mfumo wa Jua kuna sayari ngapi? Zitaje.
2. Orodhesha vitu vinavyounda Mfumo wa Jua.
3. Taja sayari iliyo mbali na Jua kuliko sayari zote.
4. Taja jina la sayari kubwa kuliko zote.
5. Ni sayari gani iliyo karibu sana na Jua?
6. Dunia ni sayari ya ngapi toka kwenye Jua?

## Kazi ya kufanya

Andaa kifani cha Mfumo wa Jua. Jua liwe katikati, tumia karatasi kutengeneza maduara ya maumbo mbalimbali ya sayari. Unaweza kuweka obiti kwa kutumia uzi au kamba. Kumbuka Jua litakuwa kubwa lenye rangi ya njano na nyekundu.

**Kumbuka:** Hii ni kazi nzuri, itundike darasani kwenu kuwaonesha wenzako.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 98 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vitu vinavyopatikana katika sayari Dunia

Vipo vitu vingi vinavyopatikana katika sayari Dunia. Vitu kama vile miti, mito, milima, nyasi, mawe na wanyama huunda mazingira. Mazingira huundwa na viumbe hai na visivyo hai. Vitu hivi ndivyo vinavyopatikana katika sayari Dunia.

*Tazama picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 2:** *Baadhi ya vitu vinavyopatikana katika sayari Dunia*

### Zoezi la 2

1. Taja vitu vitano vinavyopatikana katika sayari Dunia vinavyoonekana katika picha.
2. Ni vitu gani vingine vinavyopatikana katika sayari Dunia?
3. Taja baadhi ya vitu vilivyopo katika eneo unaloishi.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 99 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Dunia ni sayari pekee yenye viumbe hai kati ya sayari zote zinazolizunguka Jua. Anga lake ni jepesi kwa wastani likiwa na hewa. Hewa huwezesha viumbe hai kuishi. Hewa iliyoko angani ni mkusanyiko wa gesi mbalimbali. Mfano wa gesi hizo ni haidrojeni, oksijeni, kabonidayoksidi na nitrojeni. Pia, kwenye sayari Dunia kuna maji ambayo ni muhimu kwa viumbe hai. Zaidi ya robo tatu ya Dunia ni maji.

Hapo zamani babu zetu walidhani Dunia ni tambarare. Tafiti za kisayansi zimedhihirisha kuwa umbo la Dunia ni mviringo mithili ya yai. Pia, sayari Dunia ina mizunguko miwili. Dunia kujizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kulizunguka Jua.

Katika Dunia hupatikana vitu vyenye uhai na visivyo na uhai. Mfano wa vitu visivyo na uhai ni pamoja na bahari, majengo, mawe, milima na mabonde. Vilevile, mito, anga, maziwa, ardhi na hewa. Vitu vilivyo na uhai ni pamoja na wanyama, mimea, wadudu, ndege, samaki na binadamu. Sayari Dunia inapendeza katika Mfumo wa Jua.

## Zoezi la 3

1. Dunia ina mizunguko mingapi? Ni ipi hiyo?
2. Je, Dunia ina umbo gani?
3. Maji yana umuhimu gani kwa viumbe hai?
4. Kwa nini Dunia ni sayari pekee yenye viumbe hai?

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 100 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Unaweza kujikumbusha kwa kuimba shairi lifuatalo:

1. *Dunia hujizungusha,*
   *Dunia hujizungusha,*
   *Kila siku, kila siku,*
   *Kwenye mhimili wake.*

2. *Dunia hulizunguka,*
   *Dunia hulizunguka,*
   *Mara moja kila mwaka,*
   *Huzunguka Jua lake.*

**Vyanzo vya mwanga wa asili katika mazingira**

*Tazama picha hizi, kisha soma majigambo kati ya Jua, Mwezi na kimondo***.**

a. b. c.



**Kielelezo namba 3:** *Vitu vinavyotoa mwanga angani*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 101 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma majigambo kati ya Mwezi, Jua na kimondo, kisha jibu maswali.**

**Mwezi:** Mimi ndiyo Mwezi, satelaiti ya asili. Najivunia ukubwa, hakuna wa kunifikia.

**Jua:** Mwezi! Acha maringo yako! Unajivunia ukubwa gani? Hata Dunia humfikii! Eheee! Hebu nione mimi. Wewe na wenzako wote mnanizunguka. Mimi ndio mkubwa wenu.

**Mwezi:** Ukubwa! Ukubwa kitu gani? Unaweza ukawa mkubwa na bado ukawa mvivu. Ona unamulika mchana na usiku unalala. Wakati wewe umelala, mimi nampa Dunia mwanga wa asili. Shahidi ni Dunia kwa jinsi anavyonipenda. Wewe usinionee wivu. Ninampa mwanga wakati wa usiku, tena mwanga usioumiza.

**Jua:** Haha hahaa! Kweli mwezi unachekesha. Nikuulize huo mwanga unaompatia Dunia unautoa wapi? Kwa taarifa yako mimi ndiyo chanzo cha mwanga wako na wa Dunia. Pia, nawapa nishati ya umeme na joto. Mwezi usijisifu, naijua siri yako. Usiku unaakisi mwanga wangu na kuupeleka kwa Dunia.

**Kimondo:** Sawa! Nimewasikia, ninyi nyote mna sifa zenu lakini hamnishindi mimi. Mimi ndio Kimondo hakuna anayeweza kunichezea. Kati yenu hakuna anayefika duniani. Jua ndio usiseme uko mbali na binadamu. Mimi nikifika duniani, binadamu hunifanya kivutio chake cha utalii. Kama hunijui waulize watu wa Mbozi, wanavyopata pesa kwa ajili yangu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 102 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jua:** Hahahaa! Kumbe hamnijui vizuri. Mimi ndiyo Jua, nyota iliyo karibu zaidi na Dunia. Mimi ndiyo baba na mama yenu. Halafu eti nitembee. Nitembee! Nitembee kwenda wapi? Nikatafute nini? Mimi nina uwezo wa kujitengenezea mwanga, nishati na joto. Ninyi hamuwezi ng'o! Ndiyo maana kutwa mnanizunguka mkiniimbia nyimbo za kunisifu.

**Mwezi:** Aah! Waapii, mimi namzunguka Dunia kutoka Magharibi kwenda Mashariki. Mzunguko wangu binadamu hupata kuhesabu siku za Mwezi.

**Kimondo:** Ooh! Nani asiyenijua? Mara nyingine napita kwa kasi angani na kuungua. Nikiungua natoa mwanga wa kushangaza. Binadamu hufurahia kwa kunitazama.

**Jua:** Kama hamnikubali basi! Mimi ninasaidia mimea kujitengenezea chakula chake. Pia, nampa binadamu vitamin D. Hivi kwa nini hamtaki kukubali kuwa mimi ni muhimu kuliko ninyi nyote?

**Kimondo:** Mmh! Mwezi tukubali au tukatae, Jua ni nyota njema. Tazama ni nyota pekee aliye karibu yetu, nyota nyingine ziko mbali nasi.

**Mwezi:** Haya! Tukubali tu Jua ni muhimu kwetu na kwa Dunia. Naye akubali pia kuwa na sisi ni muhimu. Kwa hiyo sisi sote tuna umuhimu.

**Jua:** Ndiyo, na mimi ninakubali kuwa tuna umuhimu wetu. Wote ni bora katika maisha ya mwanadamu.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 103 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Taja vitu vinavyotoa mwanga wa asili.
2. Chanzo kikuu cha nishati ya mwanga wa asili ni kipi?

*Angalia picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 4:** *Umuhimu wa mwanga wa asili*

## Zoezi la 5

1. Unaona nini katika picha hiyo?
2. Mwanga wa Jua hutumika kwa matumizi gani katika mazingira unayoishi?
3. Unafikiri ni wakati gani watu hufanya kazi zao kwa urahisi? Kwa nini?
4. Kwa nini mwanga wa Mwezi ni hafifu kuliko mwanga wa Jua?
5. Unadhani ni kwa nini mwanga wa Mwezi hauna joto?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 104 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tofauti kati ya mwanga wa Jua na Mwezi

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Mwezi na Jua vyote hutupatia mwanga katika Dunia. Wakati wa mchana, mwanga huwa mkali. Mwanga huu hupatikana kutoka kwenye nyota iitwayo Jua. Mwanga huo husababisha Mwezi kutoonekana mchana.

Watu hutumia mwanga wa Jua kufanya shughuli zao za kila siku. Hii ni kwa sababu Jua hutoa mwanga wa kutosha. Mwanga wa Mwezi ni hafifu na hutumika wakati wa usiku. Mwanga huo hutokea pale Jua linapomulika upande mwingine wa Dunia.

Mwanga wa Jua una nguvu kubwa tofauti na mwanga wa Mwezi. Mwezi unaakisi mwanga wa Jua kumulika Dunia wakati wa usiku. Joto la Jua husaidia kutengeneza mvua wakati mwanga wa Mwezi hauwezi kusaidia kutengeneza mvua. Vilevile, nishati ya Jua hutumika na mimea kutengeneza chakula chake. Kwa kweli, Jua ni muhimu kwa viumbe hai vilivyomo duniani.

### Zoezi la 6

1. Ni kitu gani kinaakisi mwanga na kumulika duniani wakati wa usiku?
2. Kwa nini mwanga wa Mwezi hauwezi kutengeneza nishati ya joto?
3. Nyota gani hutoa mwanga mkali wakati wa mchana?
4. Taja tofauti tatu za Jua na Mwezi.

### Kazi ya kufanya

Jadiliana na wenzako kuhusu nini kingetokea kama kusingekuwepo na Jua. Andika majibu kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja faida nne za Jua.
2. Eleza kitu kipya ulichogundua baada ya kusoma Mfumo wa Jua.
3. Eleza faida za Jua, Kimondo na Mwezi kwa binadamu.
4. Taja sayari kwa mfuatano kuanzia ile iliyo karibu na Jua hadi ile iliyo mbali na Jua.
5. Eleza utakavyotumia maarifa uliyoyapata kuhusu Mfumo wa Jua katika maisha yako ya kila siku.
6. Chora Mfumo wa Jua na uandike majina yake.

*Oanisha* **kifungu A** *kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye* **kifungu B**.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| 7. Jua________ | (a) sayari kubwa kuliko zote |
| 8. Dunia__________ | (b) sayari iliyo mbali zaidi na Jua |
| 9. Sumbula ________ | (c) chanzo cha mwanga duniani |
| 10. Kausi _________ | (d) sayari yenye uhai |
| 11. Zebaki ________ | (e) vitu katika Mfumo wa Jua |
| 12. Nane ________ | (f) sayari ya nne kutoka Jua |
| 13. Obiti _________ | (g) njia ya Dunia kulizunguka Jua |
| 14. Mirihi ________ | (h) sayari iliyo karibu sana na Jua |
| 15. Asteroidi, Kometi na Meteroidi __________ | (i) idadi ya sayari |
| 16. Sarateni _________ | (j) sayari Kibete |
| | (k) sayari yenye pete baada ya sayari Sumbula |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

17. Kimondo ni chanzo cha mwanga duniani.__________
18. Mfumo wa Jua una sayari kumi.____________
19. Njia ya sayari kulizunguka Jua huitwa Obiti.__________
20. Sayari yenye pete huitwa Mirihi.____________
21. Jua huzunguka Dunia wakati wa usiku.____________

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Akisi: | kurudisha mionzi ya mwanga kutoka kwenye kitu chenye sura laini |
| Mhimili: | mstari wa kubuni ambao Dunia huegemea |
| Nishati: | uwezo wa kufanya kazi na kusababisha mabadiliko |
| Satelaiti: | kitu cha asili kinachozunguka Dunia au sayari nyingine kwa mfano Mwezi |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 107 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Rasilimali zetu

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza namna ya kuzitunza rasilimali za familia na shule. Pia, ulijifunza faida za kutunza rasilimali. Katika sura hii, utajifunza kuainisha rasilimali zilizoko katika kijiji au mtaa na kata. Vilevile, utajifunza namna ya kuthamini rasilimali zilizopo katika wilaya yako.

### Rasilimali zetu katika mji/kijiji

Kuna rasilimali mbalimbali katika kijiji au mji. Rasilimali hizo hutumika katika mazingira ya kijiji au ya mji. Zikitumika na kutunzwa vizuri tutapata matokeo mazuri ya kimaendeleo.

Fuatilia mazungumzo kati ya Rehema na Baraka, linganisha na rasilimali zinazopatikana katika kijiji au mtaa wako.

**Baraka:** Habari gani Rehema!

**Rehema:** Nzuri Baraka. Na wewe je?

**Baraka:** Ni njema tu! Japo nina uchovu kidogo.

**Rehema:** Uchovu wa nini Baraka?

**Baraka:** Tulikuwa tukikarabati jengo la mtaa wetu. Hakika ilikuwa kazi nzito sana, iliyochukuwa siku nzima.

**Rehema:** Pole sana kaka Baraka. Hongereni kwa kuzijali

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 108 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

rasilimali zenu. Sisi pia tunayo desturi ya kufanya hivyo, ndio maana tuna rasilimali nyingi sana.

**Baraka:** Rehema, umesema kwamba ninyi mna rasilimali nyingi. Ni zipi hizo?

**Rehema:** Kijiji chetu kina rasilimali mbalimbali kama vile duka, nyumba na vyombo vya usafiri. Pia, tunayo mifugo, misitu, mito, madini na ardhi.

**Baraka:** Hongera sana! Kwa mazingira ya kijijini rasilimali hizi mnazitumiaje na zinawasaidiaje?

**Rehema:** Kwa kweli zinatusaidia sana. Tunatumia rasilimali zetu katika mambo mengi. Kwa mfano, vitu kama duka na mashamba ya mazao hutuongezea kipato cha familia. Vilevile, rasilimali hizi hutupatia ajira. Misitu hutupatia dawa za asili. Hali kadhalika, misitu husaidia kufanyika kwa mvua inayotusaidia wakati wa kilimo. Pia, tunapasua mbao na tunakusanya kuni na miti ya kujengea kutoka kwenye misitu yetu. Tunapata maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo yetu. Mifugo hutupatia kitoweo, mbolea na kutuongezea kipato.

**Baraka:** Sisi tuna ardhi, mabwawa ya maji, miundombinu ya umeme na misitu. Vilevile, tuna minara ya simu, majengo na viwanja vya michezo. Kwa kweli rasilimali zikitumika vizuri zinatuletea maendeleo, tunapaswa kuzitunza vizuri. Kitu kinachoshangaza ni kuwa, kuna watu wamekuwa wakizitumia vibaya rasilimali hizi. Katika kijiji chetu baadhi ya wanakijiji huchoma misitu na kutupa taka ovyo. Pia, huvuna

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 109 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

bila kibali baadhi ya rasilimali. Vilevile, huharibu vyanzo vya maji na kulisha mifugo ndani ya misitu.

**Rehema:** Ahaa! Watu wengine wabaya sana. Sote hatupaswi kuchoka kuwaelimisha. Katika kijiji chetu tunalinda rasilimali zetu kwa kuwaelimisha wanakijiji na kuweka sheria ndogondogo. Anayekiuka sheria hizo hutozwa faini. Kwa pamoja, tunapaswa kuzitunza rasilimali zetu na kuzitumia kwa uangalifu ili zisiharibike.

## Zoezi la 1

1. Je, unaweza kujenga tabia gani kutokana na mazungumzo uliyosoma?
2. Taja rasilimali tatu zilizopo katika kijiji cha akina Rehema.
3. Je, ni rasilimali gani zilizopo katika kijiji au mtaa wako? Mnazitumiaje?
4. Ni vitendo gani vinavyoharibu rasilimali katika kijiji au mtaa wako?
5. Ni hatua gani utakazochukua kama utakuta mtu anaharibu rasilimali za mtaa au kijiji chenu?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



**Kielelezo namba 1:** *Uharibifu wa rasilimali*

b.



**Kielelezo namba 2:** *Shughuli za utunzaji wa rasilimali*



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 111 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

1. Unaona nini katika picha ya kwanza na ya pili?
2. Shughuli ulizoziona katika picha ya pili zitakuwa na matokeo gani kwenye rasilimali?
3. Unashauri nini kutokana na shughuli zinazofanyika katika picha ya kwanza?

## Rasilimali za kata

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Kila kijiji au kata ina rasilimali zake. Rasilimali hizo zinaweza kumilikiwa na mtu binafsi, familia, kijiji, mtaa au kata. Kwenye kila kata, kuna rasilimali mbalimbali.

Fuatilia mazungumzo kati ya Kiba na Mary, kufahamu rasilimali zinazopatikana katika kata.




**Kielelezo namba 3:** *Mazungumzo juu ya rasilimali za kata*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 112 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Rasilimali za kata huwa ni zile zenye thamani kubwa kuliko za kijiji au mtaa. Rasilimali za kata kwa kiasi kikubwa zinaweza kufanana na zile za kijiji au mtaa. Mfano wa rasilimali za kata ni mabwawa, misitu na machimbo ya madini. Pia, kuna majengo yanayotumika kutoa huduma za jamii kama shule, mahakama na zahanati. Vilevile, kuna rasilimali kama ardhi, samani na mito. Pia, kuna rasilimali kama maduka, magari, maegesho ya magari na mapori ya wanyama.

Kuna vitendo vingi vinavyosababisha uharibifu wa rasilimali. Vitendo hivyo ni pamoja na ujenzi wa nyumba au kulima karibu na vyanzo vya maji. Ufugaji wa mifugo mingi katika eneo moja na kutupa taka. Pia, kukata miti ovyo na kuchoma misitu vinachangia kuharibu rasilimali. Vilevile, uchimbaji madini usiotumia vifaa vya kitaalamu na kilimo cha kuhamahama kinachangia katika uharibifu wa rasilimali. Vitendo hivi, hurudisha nyuma maendeleo ya sehemu husika. Hivyo ni muhimu kutunza rasilimali zetu. Tuzitunze ili zitutunze.

Watu wote katika kata wana jukumu la kutunza na kulinda rasilimali zao ili zisiharibiwe. Rasilimali za kata zinaweza kulindwa na kutunzwa kwa namna mbalimbali. Mfano, kujenga mbali na vyanzo vya maji. Pia, kuwaelimisha watu, kuweka walinzi maalumu na kuzilinda rasilimali zetu kwa pamoja.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 113 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Ni rasilimali gani za asili unazozifahamu?
2. Ni vitendo gani vya uharibifu wa rasilimali vinavyofanyika katika kata yako?
3. Jukumu la kutunza rasilimali za kata ni la nani? Kwa nini?
4. Tufanye nini ili kutunza rasilimali za kata yetu?

**Kazi ya kufanya**

Wewe pamoja na wenzako, mkiongozwa na mwalimu wenu, tembeleeni ofisi za kata zilizopo karibu na shule yenu. Kisha kila mmoja aorodheshe rasilimali zinazopatikana katika kata hiyo.

## Rasilimali za wilaya yetu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Katika wilaya yetu tuna rasilimali mbalimbali. Rasilimali hizi zinatusaidia katika maisha yetu ya kila siku. Rasilimali hizo ni kama vile machimbo ya mchanga, vituo vya mabasi na mabango ya matangazo. Pia, yapo maduka, viwanda, ardhi, masoko, mito na mabwawa. Vilevile, kuna rasilimali nyingine kama barabara, maji, umeme na minara ya simu. Rasilimali hizi zinahitaji kutunzwa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wilaya na taifa kwa ujumla.

Ardhi ni rasilimali muhimu katika maendeleo yetu kwa sababu ndiyo inayobeba rasilimali nyingine. Tunaitumia kwa kilimo,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kujengea miundombinu kama barabara, reli na majengo. Majengo hayo tunayatumia kwa ajili ya biashara na makazi. Barabara hutumika kwa shughuli za usafirishaji. Pia, ardhi ina madini, vyanzo vya maji na mandhari mbalimbali.

Rasilimali nyingi zina changamoto za utunzaji wake. Changamoto kubwa ni uharibifu wa vyanzo vya maji na hewa. Uharibifu huo husababisha kuenea kwa magonjwa yanayowapata binadamu na mifugo. Uharibifu mwingine ni uchafuzi wa mazingira kama vile uchomaji moto misitu na ukataji miti ovyo.

Tunatunza rasilimali za wilaya yetu kwa kuziwekea ulinzi zisiibiwe au kutoharibiwa. Tunalinda vyanzo vya maji na miundombinu kama vile barabara, reli na nguzo za umeme. Tunazuia ukataji wa miti ovyo, tunapanda miti ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Pia, tuna utaratibu wa kusafisha mazingira kila mwisho wa mwezi.

**Zoezi la 4**

1. Wilaya unayoishi inaitwaje?
2. Taja rasilimali tano zinazopatikana katika wilaya yenu.
3. Ni faida gani zitokanazo na rasilimali katika wilaya yenu?
4. Je, ni vitendo gani vinavyochangia uharibifu wa rasilimali za wilaya unayoishi?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na mwalimu wa somo la Maarifa ya Jamii kuhusu rasilimali za wilaya na faida zake.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja njia tatu za kutunza rasilimali.
2. Kitu gani kinaweza kutokea kama rasilimali za kata na wilaya hazitatunzwa vizuri?

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

3. Majengo, mifugo, samani na nguzo za simu ni baadhi ya rasilimali.______________
4. Barabara hutumika kwa shughuli za uvuvi, kilimo, biashara na ufugaji.______________
5. Watu ni rasilimali.________________
6. Panga, rungu, upinde na mshale ni silaha za jadi zinazoweza kutumika kulinda rasilimali zetu.______________
7. Siyo vema kuzifanyia ukarabati rasilimali mara tu zinapoharibika.______________
8. Ardhi ni rasilimali inayotumika kwa kilimo, na ujenzi wa barabara, reli na majengo.________________
9. Mazao ya shambani ni rasilimali ambayo haiongezi mapato katika kijiji.______________
10. Mbao, kuni, mkaa na dawa za asili ni mazao yatokanayo na misitu.______________
11. Tusipozitunza vizuri rasilimali tutapata maendeleo.______
12. Kuchoma miti, kutupa taka ovyo na kuharibu vyanzo vya maji ni vitendo vinavyoharibu rasilimali.______________

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 116 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Oanisha sentensi kutoka* **safu B** *na maneno sahihi kutoka* **safu A** *ili yalete maana sahihi*

| **Kifungu A** | **Kifungu B** |
| --- | --- |
| 13. Ardhi, mito na madini____ | (a) njia mojawapo ya kutunza rasilimali |
| 14. Ajira, biashara_________ | (b) rasilimali |
| 15. Kukarabati_________ | (c) chanzo cha maji |
| 16. Barabara, majengo na nguzo za umeme______ | (d) shughuli inayoharibu rasilimali |
| 17. Kukata miti_________ | (e) fursa zinazotokana na matumizi ya rasilimali |
| | (f) huduma za jamii |

**Msamiati**

| | |
| --- | --- |
| Kukarabati: | tengeneza kitu kilichoharibika ili kifae tena kwenye matumizi |
| Miundombinu: | maumbo ya msingi na miundo ya kiasasi kama vile barabara, reli, simu na anga |
| Samani: | vifaa kama vile meza, viti, kabati, kitanda na dawati vilivyotengenezwa kwa mbao |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 117 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Uzalishaji mali

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza shughuli za uzalishaji mali zinazofanyika katika familia. Ulijifunza pia wajibu wa kila mwanafamilia katika shughuli za uzalishaji mali. Katika sura hii, utajifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali katika kijiji au mtaa na kata. Vilevile, utajifunza vikwazo vinavyojitokeza katika shughuli za uzalishaji mali.

### Shughuli za uzalishaji mali katika kijiji au mtaa

Umejifunza kwamba katika kila kijiji au mtaa kuna rasilimali mbalimbali. Watu hutumia rasilimali hizo katika shughuli za uzalishaji mali ambazo huwapatia kipato.

*Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 118 30/07/2021 11:55

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

b.



c.



**Kielelezo namba 1:** *Shughuli za uzalishaji mali*



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 119 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Ni shughuli gani za uzalishaji mali unazoziona katika picha?
2. Taja shughuli za uzalishaji mali zinazofanyika shuleni kwenu.

**Soma hadithi hii, kisha jibu maswali.**

Mwira na Mbwilo ni marafiki wanaoishi katika Kijiji cha Kitagata. Kijiji hiki kina wakazi wengi ambao hujishughulisha na kilimo cha mazao. Hivyo wanakijiji hujipatia mazao mengi. Mazao yao hutumika kwa chakula na mengine huuzwa na kujipatia fedha.

Pamoja na kilimo cha mazao, Mbwilo anafuga ng'ombe, kuku na mbuzi. Mbwilo ni mfugaji maarufu hapo kijijini. Huuza nyama ya ng'ombe, maziwa na kuku. Hakika Mbwilo ni mfanyabiashara mashuhuri pale kijijini.

Wakati huo, Mwira naye hujishughulisha na shughuli za uvuvi. Yeye huvua samaki katika bwawa lililopo hapo kijijini. Samaki hao huwatumia kwa kitoweo na wengine huwapeleka sokoni kuuza. Mwira hutumia usafiri wa bodaboda kupeleka samaki wake sokoni. Soko hilo, hutumiwa na wafanyabiashara wengi.

Kijiji hiki kina rasilimali za misitu yenye ndege na wanyama mbalimbali wa kuvutia. Watu kutoka sehemu mbalimbali hutembelea Kijiji cha Kitagata ili kuona ndege, nyani, ngedere na sokwe. Watu hao huitwa watalii. Kijiji hiki hujipatia pesa nyingi kutokana na utalii. Watalii wanapofika kijijini hapo, hulala

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

katika nyumba za wageni. Wenye nyumba hizo hujipatia pesa kutokana na malazi na chakula wanachowauzia watalii.

Baadhi ya wanakijiji hujishughulisha na upasuaji wa mbao katika misitu iliyopo hapo kijijini. Kisha huzisafirisha kutoka porini hadi kijijini. Baadaye huzipeleka mjini kwa usafiri wa malori ya kukodi. Mwira ana kiwanda chake cha kutengeneza samani. Yeye hutoa mbao porini na kutengeneza viti na vitanda. Pia, hutengeneza makabati ya vyombo na samani nyingine.

## Zoezi la 2

1. Orodhesha shughuli za uzalishaji mali zinazotajwa katika hadithi uliyoisoma.
2. Ni shughuli gani za uzalishaji mali zinazofanywa na wakazi wa kijiji au mtaa wenu?
3. Eleza faida unazoweza kupata kutokana na kufanya shughuli za uzalishaji mali.
4. Taja shughuli nne za uzalishaji mali zinazofanywa na wakazi wengi wa Kijiji cha Kitagata.
5. Wewe unapenda shughuli gani za uzalishaji mali? Kwa nini?

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako, kutembelea kijiji au mtaa ulio karibu na shuleni kwenu. Kila mmoja aorodheshe shughuli za uzalishaji mali zinazofanyika hapo kijijini au mtaani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mahitaji ya kijiji au mtaa

Soma habari katika mchoro wa picha hizi, kisha jibu maswali.

*Naitwa **John,** natokea Kijiji cha Maringeni. Kijijini kwetu tuna changamoto ya usafiri hivyo tunahitaji barabara nzuri. Vilevile, tunahitaji shule kwani watoto hutembea umbali mrefu kwenda shule.*

*Naitwa **Manka,** natoka Kijiji cha Mbokomu. Kwetu tunahitaji maji ya bomba ili kuwaondolea wanakijiji shida ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji. Pia, tunahitaji zahanati ili kupata huduma ya afya. Vilevile, tunahitaji eneo la kuuzia bidhaa zetu.*



*Naitwa **Habibu,** natoka Mtaa wa Mazengo. Mtaa wetu kwa sasa hauna umeme. Tukipata umeme nitaweza kusoma vizuri usiku. Pia, nikiwa mkubwa nitafungua biashara ya kuuza vinywaji baridi na mtandao wa mawasiliano.*

**Kielelezo namba 2:** Mahitaji ya kijiji au mtaa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jaza mahitaji katika jedwali lifuatalo. Tumia taarifa ulizosoma kutoka kwenye kielelezo namba 2. Nafasi moja imejazwa kama mfano.

| **Mahitaji** | **Kijiji cha Maringeni** | **Kijiji cha Mbokomu** | **Mtaa wa Mazengo** | **Jaza mahitaji ya kijiji au mtaa wako** |
|---|---|---|---|---|
| Barabara | | | | |
| Shule | | | | |
| Maji | | *Maji* | | |
| Umeme | | | | |
| Zahanati | | | | |

## Shughuli za uzalishaji mali katika kata

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

Binadamu hujishughulisha na kazi mbalimbali ili kujipatia kipato. Kazi hizi ni kama vile kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini. Pia, zipo shughuli nyingine kama uvuvi, viwanda na biashara.

Watu hulima mazao kama vile mahindi, maharage, mpunga na viazi. Mazao haya huitwa mazao ya chakula. Aidha, hulima mazao ya biashara kama kahawa, pareto, mkonge na chai. Mazao hayo hupelekwa moja kwa moja viwandani kwa ajili ya

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kutengeneza bidhaa. Vilevile, watu hujishughulisha na ufugaji wa mbuzi, kondoo, ng`ombe, punda, kuku na bata. Watu wanaojishughulisha na shughuli hizo huitwa wafugaji. Ufugaji ni sehemu ya uzalishaji mali. Kuna jamii nyingine hujishughulisha na uvuvi.

Uchimbaji wa madini ni shughuli mojawapo ya uzalishaji mali. Shughuli hii hufanyika kwa kuchimba madini ardhini. Watu huchimba miamba na kupata madini mbalimbali. Mahali madini yanapochimbwa, panaitwa mgodi. Madini ni mawe yenye thamani yatumikayo kama malighafi. Zipo aina nyingi za madini kama vile almasi, dhahabu, shaba, tanzanaiti, fedha, ulanga, chumvi na chuma.

Shughuli za uzalishaji mali ni muhimu katika kukidhi mahitaji mbalimbali ya wanakata. Mahitaji hayo ni huduma za afya, elimu, maji safi, umeme na zahanati. Vilevile, huwapatia ajira na kipato kinachowawezesha kujikimu kwa kupata huduma bora za jamii. Ama kweli, shughuli za uzalishaji mali ni ukombozi katika maisha ya wanakata.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya kufanya**

Tembelea ofisi za serikali ya kata yenu kisha:

(a) Uliza rasilimali zilizopo katika kata yenu.
(b) Uliza mahitaji ya kata hiyo.
(c) Kwa kushirikiana na wenzako tembeleeni maeneo yenye shughuli za uzalishaji mali mkiongozwa na mwalimu. Mbaini jinsi shughuli hizo zinavyofanyika kijijini au mtaani kwenu.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 124 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Tazama picha hii, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 3:** *Wanafunzi na mwalimu wakitembelea soko*

## Zoezi la 3

1. Ni shughuli gani unazoziona zikifanyika katika picha hapo juu?
2. Kwa nini wanafunzi walitembelea soko hilo?
3. Unafikiri ni faida gani wanafunzi walizozipata katika matembezi hayo?
4. Je, wewe umewahi kutembelea shughuli yoyote ya uzalishaji mali?
5. Ikitokea umetembelea soko la kijijini au mtaani kwako, ni maswali gani utakayouliza?



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 125 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andaa maswali utakayouliza kuhusu shughuli za uzalishaji mali kwa mwalimu wa somo hili. Kisha andika taarifa uliyoipata katika daftari lako na uisome darasani.

## Vikwazo katika uzalishaji mali

Katika sehemu iliyopita, umejifunza kuwa watu wengi hujishughulisha na uzalishaji mali. Uzalishaji huo hufanyika katika vijiji, mitaa na kata. Katika sehemu hii utajifunza jinsi ya kukabiliana na vikwazo mbalimbali katika uzalishaji mali. Ukubwa wa vikwazo hivyo huwa tofauti kati ya ngazi mbalimbali. Kwa mfano, kuanzia ngazi ya mtu binafsi na mwingine hadi ngazi ya taifa.

**Soma shairi, kisha jibu maswali.**

1. *Ndugu zangu karibuni, vikwazo kuwaeleza,*
*Ardhi kuwa vitani, hasara kujitokeza,*
*Mazingira hatarini, uchumi kuangamiza,*
*Na wote tuwe salama, uzalishaji fufua.*

2. *Zana duni za kilimo, tatizo tena jamani,*
*Mali zetu zilizomo, zimekuwa matatani,*
*Na masoko yaliyomo, hayakidhi asilani,*
*Na wote tuwe salama, uzalishaji fufua.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. *Utunzaji mazingira, ni jukumu letu sote,*
*Misitu yetu imara, ni faida kwetu wote,*
*Kupata mavuno bora, ni furaha yetu sote,*
*Na wote tuwe salama, uzalishaji fufua.*

4. *Serikali za vijiji, maeneo yatengeni,*
*Weka gari la kijiji, mazao fika sokoni,*
*Wezesha wazalishaji, mabenki wakopesheni,*
*Na wote tuwe salama, uzalishaji fufua.*

**Zoezi la 4**

1. Kutokana na shairi ulilosoma, taja vikwazo vitano vinavyokabili uzalishaji mali.
2. Katika kijiji au mtaa wenu kuna vikwazo gani vinavyokabili uzalishaji mali?
3. Eleza njia zinazoweza kutumika kutatua vikwazo vya uzalishaji mali.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Pendekeza njia tatu za kukabili vikwazo vya uzalishaji mali katika kata yako.
2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika kifungu cha habari kwa kutumia maneno yaliyo katika jedwali.

**mahindi, maharage na ndizi; ukataji wa miti; ukame; shughuli za uzalishaji; kahawa na katani; ardhi kukosa rutuba.**

Shamba ni mahali ambapo watu hufanya _____. Wakulima huzalisha mazao kama ___________________. Kunapokuwa na uhaba wa mvua _______ hutokea. Kilimo holela huweza kusababisha ______. Katika mazingira yetu _____ husababisha upungufu wa mvua na ongezeko la joto.

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Gulio: | soko la nje ambalo hufanywa kwa siku maalumu |
| Madini: | vito na mawe au miamba yenye thamani inayopatikana chini ya ardhi |
| Malighafi: | mali ambayo hutumika kutengeneza kitu kingine |
| Mgodi: | eneo la ardhi panapofanyika shughuli za kuchimba madini |
| Mtandao: | mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki unaopitia katika kompyuta au simu za mkononi |
| Utalii: | utembeleaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya kujifunza na kujifurahisha |
| Uzalishaji mali: | shughuli ya kuzalisha bidhaa ili kujipatia kipato |
| Vikwazo: | kizuizi cha jambo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 128 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Fursa katika maeneo mbalimbali

Ulipokuwa Darasa la Tatu, ulijifunza shughuli za kiuchumi sehemu zenye ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha. Katika sura hii, utajifunza fursa zilizopo sehemu zenye mbuga za wanyama. Vilevile, utajifunza fursa zilizopo sehemu zenye madini na misitu. Hali kadhalika, utajifunza jinsi ya kuzitumia fursa hizo.

### Fursa zilizopo katika maeneo ya uchimbaji madini

Angalia picha ifuatayo ili utambue baadhi ya madini mbalimbali yanayopatikana nchini Tanzania.




**Kielelezo namba 1:** *Picha za madini*



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 129 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sehemu zenye madini zina fursa nyingi. Baadhi ya fursa hizo ni uchimbaji wa madini ambao huwapatia watu ajira. Vilevile, kuna fursa ya biashara ya kuuza chakula na bidhaa nyingine kama hereni, bangili na nguo. Katika sehemu zenye uchimbaji wa madini pia watu hufanya kazi za usafirishaji.

*Soma jedwali lifuatalo kutambua maeneo ya Tanzania ambayo yana madini mbalimbali.*

| **Madini** | **Mahali** |
|---|---|
| (i) Almasi | Mwadui na Maganzo katika mkoa wa Shinyanga |
| (ii) Dhahabu | Biharamulo, Chunya, Buhemba, Kahama, Tarime na Geita |
| (iii) Tanzanaiti | Mererani katika mkoa wa Manyara |
| (iv) Ulanga | Ulanga mkoani Morogoro na Mpanda mkoani Katavi |
| (v) Bati | Karagwe mkoani Kagera |
| (vi) Chuma | Liganga wilaya ya Ludewa mkoani Njombe |
| (vii) Chumvi | Mwambao wa Bahari ya Hindi katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi na Uvinza mkoani Kigoma |
| (viii) Fosfeti | Liganga wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, Minjingu karibu na Ziwa Manyara |
| (ix) Chokaa | Tanga na Mbeya |
| (x) Makaa ya mawe | Ngaka mkoani Ruvuma, Kiwira, Chunya na maeneo ya Ziwa Rukwa, Mchuchuma na wilaya ya Ludewa mkoani Njombe |
| (xi) Uraniamu | Namtumbo mkoani Ruvuma na Manyoni mkoani Singida |

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 130 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maeneo ya mgodi

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*

a.



b.



**Kielelezo namba 2:** *Shughuli za kiuchumi sehemu zenye madini*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Ni shughuli gani za kiuchumi zinazoonekana katika picha?
2. Je, wananchi wanaoishi karibu na migodi wanapata fursa gani?
3. Ni shughuli gani unazopenda kufanya kati ya hizi zinazoonekana katika picha?
4. Taja faida tano tunazozipata kutokana na madini.
5. Tunapata vitu gani kutoka kwenye migodi?

## Fursa zilizopo kwenye maeneo yenye misitu

Shughuli mbalimbali za kiuchumi hufanyika katika sehemu zenye misitu na mbuga za wanyama. Zipo fursa kadhaa kwenye maeneo ya misitu. Fursa hizi ni urinaji wa asali pamoja na uwindaji wa wanyama mbalimbali. Ili uweze kufanya uwindaji, inabidi upate kibali kutoka serikalini. Pia, tunapata miti ambayo hutumika katika kazi mbalimbali kama ulivyosoma katika sura iliyotangulia. Vilevile, miti hutumika kama malighafi za kupata dawa za binadamu na viumbe wengine. Misitu ina majani na matunda yanayofaa kwa chakula cha binadamu na viumbe wengine.

Nchi ya Tanzania ina maeneo mengi yenye misitu. Kwa mfano, msitu wa Usambara mkoani Tanga na msitu wa Mdandu mkoani Njombe. Ipo pia misitu ya Biharamulo, Rubya na Misenyi mkoani Kagera. Vilevile, ipo misitu ya Uluguru na Mahenge mkoani Morogoro na Mabwepande mkoani Dar es Salaam. Misitu hii ni maliasili na kivutio cha taifa.

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 132 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Tazama picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 3:** *Fursa zilizopo maeneo yenye misitu*

## Zoezi la 2

1. Unadhani ni fursa gani nyingine za kiuchumi zinazoweza kufanyika katika msitu unaoonekana kwenye picha?
2. Ni shughuli gani utakayoweza kufanya katika eneo la misitu mara umalizapo elimu yako?

## Faida zipatikanazo sehemu zenye misitu

Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.

1. *Mimi ndiye maarufu, watu wote wanijua,*
*Jina langu maarufu, ni msitu mwanijua,*
*Watu wengi hunisifu, kwa faida nazotoa,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

FOR ONLINE USE ONLY



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 133 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. *Hewa safi naitia, viumbe waitumia,*
*Viumbe hai tumia, amani mwajipatia,*
*Hakuna wa kujutia, maisha mwafurahia,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

3. *Mvua nyingi zanyesha, mimi nazitengeneza,*
*Maji nayatiririsha, viumbe hai kukuza,*
*Hayawi mema maisha, wanangu ninawajuza,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

4. *Mbao mwazifurahia, kila pande mwatumia,*
*Viti, milango undia, kabati na meza pia,*
*Vivuli mwavitumia, matunda nawapatia,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

5. *Fursa nyingi zijua, kwenu bora zitumia,*
*Uchumi kuuinua, mimi kuniangalia,*
*Kuwinda mbinu kujua, nyama wanajipatia,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

6. *Nimezitoa ajira, vijana wadogo pia,*
*Waishi maisha bora, faida kufurahia,*
*Msiyafanye madhara, kukata bila ridhia,*
*Nitunze mnithamini, mimi ni faida kwenu.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Taja mazao mbalimbali yanayotokana na misitu.
2. Nini faida ya misitu katika kijiji au wilaya yenu?

### Fursa zilizopo maeneo yenye mbuga za wanyama

Wanyama pori hupatikana kwa wingi katika mbuga za wanyama. Wanyama hao ni kama vile tembo, simba, nyati, swala, sungura, pundamilia na twiga. Pia, wapo chui, digidigi, mbweha, faru, kiboko, nyani na wanyama wengine mbalimbali.

Baadhi ya mbuga za wanyama nchini Tanzania ni Manyara, Mikumi, Saadani, Serengeti, Ruaha, Gombe na Kisiwa cha Rubondo. Hakika tumejaliwa fursa mbalimbali katika maeneo haya. Tukiyatunza na kuyatumia vizuri yatatuletea pesa na kutuondolea umaskini.

*Tazama picha ifuatayo, kisha jibu maswali.*



**Kielelezo namba 4:** *Fursa zilizopo maeneo yenye mbuga za wanyama*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Taja fursa unazoziona katika picha.
2. Je, ni fursa gani zinazoweza kuwepo maeneo yenye mbuga za wanyama ambazo hazipo kwenye picha?
3. Taja mbuga tano za wanyama unazozijua hapa Tanzania.
4. Unawaona wanyama wa aina ngapi katika picha? Wataje.
5. Ni mnyama gani amekuvutia zaidi? Kwa nini?

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako pamoja na mwalimu wa somo kutembelea mojawapo ya sehemu zifuatazo;

(a) maeneo ya migodi,
(b) mbuga za wanyama,
(c) orodhesha fursa nne (4) zinazopatikana katika sehemu hizo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari hii, kisha jibu maswali.**

Kuwepo kwa mbuga za wanyama katika maeneo mbalimbali, huchochea shughuli za kiuchumi. Watu hupata fursa ya kujenga nyumba za wageni na hoteli za kitalii kwa ajili ya kutoa huduma. Kwa hiyo, watu hupata ajira katika hoteli hizo. Pia, wapo watu ambao huajiriwa au kujiajiri kama waongoza watalii kwenda mbugani.

Wengine hufanya kazi za udereva katika magari na malori ya kitalii. Watu wengine wa karibu na mbuga huanzisha usafiri wa bodaboda. Hii husababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya usafiri wa abiria. Watu wengine huanzisha maduka na biashara ambayo huwapatia kipato. Wachongaji nao hujishughulisha na kazi za uchongaji wa vinyago na uchoraji. Vinyago hupendwa na watalii, hivyo huwapatia pesa za kujikimu. Vilevile, serikali hujipatia pesa za kigeni. Hakika mbuga za wanyama ni hazina yetu.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 5

1. Kwa nini mbuga za wanyama ni hazina muhimu kwa taifa la Tanzania.
2. Je, kama ungekuwa unaishi karibu na mbuga za wanyama ungefanya kazi gani kujipatia kipato?

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako pamoja na mwalimu wa somo kutembelea mazingira ya kijiji au mtaa. Mbaini fursa zilizopo, kisha ziorodhesheni fursa hizo na mzisome darasani.



Maarifa ya jamii STD 4 -final 3 May 18.indd 137 30/07/2021 11:56

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la jumla

**Jibu maswali haya.**

1. Taja fursa zilizopo kwenye mbuga za wanyama.
2. Bainisha vitu vinavyopatikana kwenye misitu.
3. Taja vitu vitano vinavyotokana na madini.

*Andika* **NDIYO** *kama sentensi ni sahihi na* **HAPANA** *kama sentensi si sahihi.*

4. Mbwa, nyati, sungura na simba ni wanyama wa porini.______
5. Mazao ya misitu hutumika kutengeneza milango na madirisha._________
6. Mererani ni eneo linalozalisha madini ya bati._________
7. Upinde, mkuki na mshale sio vifaa vya kupasulia mawe._______
8. Watu hupata dawa za kutibu magonjwa mbalimbali kutoka kwenye misitu._________

### Msamiati

| | |
|---|---|
| Fursa: | nafasi ya kuweza kufanya jambo |
| Mbuga: | eneo la nchi lenye nyasi nyingi, miti na vichaka vya hapa na pale |
| Ridhaa: | hiari au kibali cha kutenda jambo |

FOR ONLINE USE ONLY

**Vitabu vingine kutoka**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## Darasa la Nne



















ISBN 978-9987-09-326-7

Maarifa ya Jamii
Kitabu cha Mwanafunzi
Darasa la Nne